

Pambazuko

Toleo Namba 187

Jumatatu, Oktoba 19-25, 2026

Tunamkumbuka Nyerere kwa picha, fikra na ndoto zake? Uk. 28

Manukato hatari afya za watoto



Habari Uk. 6&7

Makonda analaumiwa kwa lipi?

KUMEZUKA mjadala mkubwa wiki iliyopita baada ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Paul Christian Makonda, kuanza ziara ya siku kadhaa mkoani Mwanza kukagua miradi ya maendeleo.

Habari Uk. 16

667,040 kufanya mtihani wa kidato cha nne leo

Uk. 20



Ndejembu akerwa kasi ndogo ujenzi wa barabara

MAKAMU wa Rais wa Tanzania, Deogratius Ndejembu, amekerwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa siku moja iliyopita ya kufungua barabara...



Habari Uk. 5

Tafakuri ya Bagonza

Labda Baba wa Taifa angesema haya...

Safu Uk. 10

Teknolojia

AI yaweza kugeuka janga kwa binadamu

Safu Uk. 27

Mgongano wa maslahi upangishaji wa Hifadhi ya Barabara ya Morogoro

Uk. 12

■ Tahariri

Sasa tuache blabla, tumuenzi Nyerere kwa vitendo

KILA inapofika Oktoba 14, Watanzania hukumbuka maisha, uongozi na mchango mkubwa wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyeongoza Tanganyika kupata uhuru na badaye kuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ni siku ambayo hotuba hutolewa, makongamano huandaliwa na mijadala mbalimbali hufanyika kuhusu falsafa, misingi na maono ya kiongozi huyo aliyefariki dunia Oktoba 14, 1999, katika hospitali moja jijini London, Uingereza.

Hakika, kumbukumbu hizo zina umuhimu mkubwa katika historia ya taifa letu. Hata hivyo, tunaamini kwamba kumuenzi Mwalimu Nyerere hakupaswi kuishia kwenye hotuba nzuri, maandamano, makongamano au kusifia uongozi wake mara moja kwa mwaka.

Tunapaswa kujiuliza swali moja muhimu; je, tunayaishi kwa vitendo yale ambayo Mwalimu Nyerere aliyapigania katika maisha yake?

Nyerere aliamini katika utu, uadilifu, usawa, haki, umoja wa kitaifa na maendeleo yanayomweka mwananchi mbele. Aliichukia rushwa, ubaguzi, unyonyaji na matumizi mabaya ya madaraka. Alisisitiza kwamba thamani ya uongozi hupimwa kwa namna unavyoboresha maisha ya watu, hasa wanyonge.

Kwa msingi huo, sisi Pambazuko tungependa kuona kila Mtanzania akimkumbuka Mwalimu kila siku, si Oktoba 14 pekee, bali kuwa utaratibu wa kila mara kwa kufanya kazi kwa ajili yafamilia na Tanzania.

Ni vyema kumkumbuka huko kuwe katika matendo yanayolijenga taifa zaidi, badala ya maneno yanayopotelea kwenye upepo baada ya sherehe kumalizika.

Mtumishi wa umma anayewahudumia wananchi kwa uaminifu, bila kudai rushwa, anamuenzi Nyerere. Mwalimu anayefundisha kwa bidii,

daktari anayemhudumia mgonjwa kwa utu na mkulima anayezalisha chakula kwa juhu-di, wote wanashiriki kutimiza maono yake.

Vivyo hivyo, mwanasiasa anayeheshimu sheria, anayekubali kukosolewa na anayesimamia haki za wananchi bila kujali itikadi zao, anatoa heshima ya kweli kwa Baba wa Taifa.

Lakini hatuwezi kudai tunamuenzi Mwalimu huku tukivumilia rushwa, ubadhirifu wa mali za umma, ukosefu wa haki, ubaguzi na vitendo vinavyodhoofisha umoja wetu.

Haiwezekani kumsifu kiongozi aliyesisitiza usawa, halafu tukakubali mazingira ambayo wachache wanafaidi rasilimali za taifa huku wananchi wengi wakihangaika kupata huduma muhimu za afya, elimu na maji safi.

Tunapaswa pia kukumbuka kwamba Nyerere hakuwa malaika. Kama binadamu na kiongozi, alikuwa na upungufu na baadhi ya sera zake zilikuwa na changamoto. Hata hivyo, uzalendo wake na dhamira ya kujenga taifa lenye mshikamano vinaendelea kutoa mafunzo muhimu.

Kwa hiyo, kumuenzi hakumaanishi kuiga kila alichofanya, bali kujifunza misingi bora aliyotuachia na kuitumia kukabiliana na changamoto za sasa.

Pambazuko tunawaomba viongozi wetu wawe mstari wa mbele kuonyesha mfano. Wasihubiri uadilifu huku matendo yao yakiipingana na wanayoyasema.

Vijana nao wajifunze historia yake na kuitafsiri katika ubunifu, uwajibikaji na uzalendo.

Tunaamini kwamba kumbukumbu bora zaidi ya Mwalimu Nyerere si ukubwa wa sherehe tunazoandaa, bali ukubwa wa matokeo ya matendo yetu katika kuboresha maisha ya Watanzania.

Tukifanya hivyo, Oktoba 14 haitakuwa siku ya kumkumbuka Nyerere kwa maneno pekee, bali kilele cha juhudi tunazofanya kila siku kulijenga taifa alilolipenda.

Mwenge wa Uhuru Sumbawanga ■



Makamu wa Rais, Deogratius Ndejimi, akikabidhiwa Mwenge wa Uhuru kwa kiongozi wa mbio hizo kitaifa mwaka 2026, Wazo Mwang'onda, wakati wa kilele cha sherehe hizo na kumbukizi ya miaka 27 tangu kufariki kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, zilizofanyika Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa mwishoni mwa wiki iliyo-pita. (Picha na OMR).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

■ Dunia: Hapa na Pale

Nyati wa maziwa wagombaniwa

ZAIDI ya wakulima 800 wamejitokeza kuwasili-sha maombi ya kutaka kununua nyati wa kufuga kwa ajili ya maziwa, ikiwa ni mkakati mpya wa kukabiliana na uhaba wa maziwa nchini Kenya.

Maziwa yamepungua kwa kiasi kikubwa nchini humo baada ya kuwepo kwa ukame, hivyo malisho ya ng'ombe kupungua na maziwa kukosekana.

Serikali imesema imekamilisha masharti ya kuwepo kwa vyeti vya afya ya mifugo vinavyohitajika kuagiza nyati hao kutoka India na kuweka wazi makubaliano kuhusu bei na gharama za usafirishaji.

Tayari zaidi ya nyati milioni 203 wanafugwa duniani na maziwa yao yana kiwango cha mafuta kinachokaribia mara tatu ya maziwa ya ng'ombe wa kawaida, ambacho huyafanya maziwa ya nyati kufaa kutengeneza bidhaa zenye thamani kubwa kama jibini, mtindi, siagi na samli.

Aogopa kutumia nyuklia Iran

RAIS wa Marekani, Donald Trump amesema hatatumia silaha za nyuklia dhidi ya Iran na kwamba hafikirii kutuma wanajeshi wake wa ardhini kushambulia nchi hiyo ya Kiarabu.

Katika mahojiano na Newsmax, Trumpe alieleza kuwa; "Hatutatumia silaha za nyuklia. Hatuhitaji kwa sasa."

Trump pia alisema Marekani inaweza kuanzisha shambulio jingine dhidi ya vituo vya nyuklia vya Iran, ikiwemo eneo la Koh Kalang, endapo ataona kuna ulazima wa kufanya hivyo.



Duterte matatani ICC

ALIYEKUWA Rais wa Ufilipino, Rodrigo Duterte (81) ambaye sasa anakabiliwa na mashtaka kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) amejikuta matatani baada ya mahakama hiyo kutangaza kuwa pamoja na utata wa afya yake, anastahili kuendelea na mashtaka.

Duterte ambaye alikuwa kiongozi wa nchi hiyo 2016-2022, anashtakiwa kwa uhalifu dhidi ya binadamu ambao aliufanya dhidi ya wapinzani wake.

Kesi yake inatarajiwa kuanza Novemba 30. Inaelezwa kuwa afya yake imetetereka akiwa anasumbuliwa na matatizo ya kupoteza kumbukumbu.

Alijitokeza mbele ya mahakama hiyo kwa mara ya kwanza Septemba mwaka huu kujibu mashitaka hayo.



Ndugu wa Tshisekedi wapekuliwa

NDUGU na washirika wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi waliopo nchini Ubelgiji, wameripotiwa kuvamiwa na kupekuliwa na vyombo vya usalama, katika uchunguzi wa tuhuma za utakatishaji fedha.

Hatua hiyo inaongeza shinikizo kwa tuhuma dhidi ya Tshisekedi kwamba watu wake wa karibu wamekuwa wakidaiwa kujilimbikizia mali ambazo hazina maelezo mazuri namna walivyopata, huku wengi wakidai, chanzo chake ni mapato ya serikali.

Wapinzani wa Rais Tshisekedi wamekuwa wakimtuhumu kuhusika na kile wanachodai kuwa ni ufisadi wa fedha za serikali kupitia kwa ndugu na jamaa zake.

Hata hivyo, kiongozi huyo amekuwa akikanusha madai hayo na kueleza kwamba ni mbinu za kisiasa kumpunguzia heshima yake.

Ndejembu akerwa kasi ndogo ujenzi wa barabara

Na Mwandishi WETU, Mbeya

MAKAMU wa Rais wa Tanzania, Deogratius Ndejembu, amekerwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa siku moja iliyopita ya kufungua barabara zilizofungwa kutokana na ujenzi.

Ndejembu amesema kufunga barabara kunaongeza adha ya usafiri kwa wananchi na kugeuka kero ambapo lawama “inatupiwika serikali nzima.”

Ameagiza kuimarishwa kwa usimamizi wa mradi huo huko Mbeya, huku akitaka hatua zichukuliwe dhidi ya watendaji wanaoshindwa kutimiza wajibu wao.

Akirejea kwa kushtukiza katika eneo la ujenzi jana, Ndejembu amebaini kuwa licha ya maagizo aliyoyatoa kwa Wizara ya Ujenzi kupitia Tanroads, baadhi ya barabara bado hazijafunguliwa na kazi haziendi kwa kasi inayotarajiwa, hali iliyomfanya kuhoji uwajibikaji wa wasimamizi wa mradi huo.

Amesema haikubaliki kwa mkandarasi aliye-lipwa takribani Shilingi bilioni 40 kuendelea na ujenzi kwa kasi isiyoendana na fedha alizopokea, huku wananchi wakiendelea kupata usumbufu.

Ndejembu amemtaka Waziri wa Ujenzi, Masanja Kadogosa, kuhakikisha Tanroads inasimamia utekelezaji wa mradi huo kwa mujibu wa mkataba na kuwachukulia hatua watendaji wanaotoa taarifa za uongo kuhusu maendeleo ya kazi.

Akionyesha kutoridhishwa na hali hiyo, Ndejembu amesisitiza kuwa serikali haitavumilia uzembe, udanganyifu na matumizi mabaya ya fedha za umma, huku akitaka watendaji wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao wondolewe na barabara zisizopitika zifunguliwe haraka ili kupunguza kero kwa wananchi mkoani Mbeya.



Makamu huyo wa rais amesisitiza kuwa serikali ya imejipanga kuhakikisha fedha za walipa kodi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa, na kwamba watendaji wenye tabia ya kudokoa dokoa hawataavumiliwa.

Kuhusu upungufu wa maji, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amesema mahitaji ya eneo la Uyole ni lita milioni 12 kwa siku, wakati uzalishaji uliopo ni lita milioni nane pekee.

Awezo amesema wakati utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji mkoani Mbeya ukiendelea, serikali itaanza kuchimba visima Jumatatu katika kata zenye upungufu mkubwa wa maji, sambamba na kuweka utaratibu wa kuwaunganishia huduma kwa mkopo wananchi wasioweza kumu-gharama za awali.

Ndejembu yuko mkoani Mbeya kwa ziara ya kikazi akitilia mkazo uwajibikaji kwa wasimamizi wa miradi ya maendeleo, kwamba fedha za umma lazima ziendane na kasi ya utekelezaji wa miradi na matokeo yanayoonekana katika masha ya wananchi, badala ya ahadi zisizotekelezwa.

■ Habari Kuu

Manukato hatari afya za watoto

Wataalamu waonya kuhusu matatizo ya kupumua; utafiti wahusicha usonji na vichanga kuvuta harufu za baadhi ya manukato (kemikali) na kuathiri ubongo.



Na Mwandishi WETU

KUMEKUWA na ongezeko la watoto chini ya miaka mitatu kuota nyama za puani (adenoid) na hata usonji, na kuelezwa na wataalamu kusababishwa na matumizi ya manukato jirani na vichaga, Pambazuko linaweza kueleza.

Wataalamu wa afya wamelithibitishia Pambazuko kuwa utumiaji wa manukato hayo na vitu vingine vinavyopenya puani kupitia mfumo wa hewa husababisha mzio (allergy) na kusababisha madhara makubwa kwa watoto hasa tatizo hilo linapochelewa kugundulika.

Mtafiti na Bingwa wa Watoto kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Profesa Karimu Manji, wakati

akiwasilisha utafiti wake kuhusu usonji mwaka 2025, alisema alibaini manukato, dawa za kupuliza kuua wadudu, zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu ubongo wa mtoto na kusababisha usonji.

Mbali na hilo, Profesa Manji pia alibaini matumizi ya simu janja, vishikwambi na runinga ambazo zinatumiwa na wazazi kama njia ya kuwaburudisha au kuwanyamazisha inachangia tatizo hilo.

Mtaalamu huyo aliwataka wazazi na wote wanaolea watoto kuwa makini na kuwaweka watoto jirani na maeneo yenye manukato hata yale yanayopakwa kwenye nguo ama vitanda vyao.

Alisema tahadhari hii ni muhimu hasa kutokana na matumizi ya manukato, mafuta yenye harufu kali na bidhaa za kusafisha au kunukisha vyumba katika mazingira ambayo watoto wadogo hukaa.

Pambazuko limezungumza na baadhi ya wazazi wenye watoto waliobainika kuwa na nyama puani na kueleza kuwa hawafahamu chanzo halisi cha ugonjwa huo.

“Mtoto wangu akilala anashindwa kupumua, baada ya kuona hali hiyo inaendelea kuwa mbaya nilimpeleka hospitali akaandikiwa kipimo cha X-ray ambapo amekutwa na vinyama vya pua ambavyo vimeshakuwa vikubwa, hivyo anatakiwa kufanyiwa upasuaji.

“Sababu sijui na sijauliza zaidi. Ninachohitaji ni mwanangu apone, sina bima ya afya na gharama za matibabu nimeambiwa ni shilingi 650,000,” amesema Asia Ferrous.

Mzazi mwingine, Salome Mushi, ameeleza; “Nimesumbuka tangu mwaka jana, awali nilidhani mwanangu ameweka kitu puani kwa sababu akiongea alikuwa kama amebana pua, kumbe ni vinyama vimeota kwenye matundu yote. Wiki iliyopita amefanyiwa upasuaji, gharama za matibabu ni kubwa nimelipa zaidi ya milioni moja.”

Inaendelea Uk. 7

Manukato hatari...

Inatoka Uk. 6

Mshauri wa masuala ya afya

Dkt. Gaudence Mathew ambaye ni tabibu wa binadamu, amezungumzia changamoto hiyo kuwa imeongezeka zaidi katika miaka ya karibuni kutokana na wazazi wengi kuwa na matumizi makubwa ya manukato.

“Suala la urembo linachangia, hasa perfume (manukato) wazazi na walezi wengi wanatumia manukato bila kujua athari zinazowapata wato wao kupitia njia ya hewa...”

“Ndio maana inashauriwa mzazi kuepuka kutumia kemikali yenye harufu zikiwamo sabuni na mafuta karibu na mtoto. Mzazi pia anapaswa kuhakikisha kuwa mtoto hakai karibu na vumbi au moshi,” anasema mtaalamu huyo.

Akizungumzia zaidi ugonjwa huo, daktari huyo amesema nyama za nyuma ya pua zina faida ya kulinda mwili dhidi ya maambukizi ya mfumo wa hewa lakini zinapozidiwa kazi huvimba.

Naye Daktari bingwa wa watoto kutoka Medinova Specialized Polyclinic, Dkt. Dea Rimoy, amesema matatizo ya nyama za pua yanahusiana na mzio, ambapo mtoto anapata mafua ya mara kwa mara na kusababisha kuta za pua kuvimba kutokana na virusi vya mafua.

“Allergy imekuwa kubwa hivi sasa. Watoto kuanzia mwaka mmoja hadi miaka kumi wanapata maumivu ya masikio, mafua na vikohozi visivyokwisha, lakini si kila mtoto mwenye mafua ana nyama za pua,” anafafanua.

Anaeleza kuwa upo uwezekano wa asilimia 90 kwa mtoto anayegundulika kuwa na nyama za pua kutofanyiwa upasuaji endapo atafikishwa hospitali mapema na kupatiwa matibabu ikiwamo kumuepusha na visababishi vya tatizo hilo.

Dkt. Dea anaeleza kuwa mbali na sababu nyingine, tatizo hilo pia linaweza kuwa la kurithi kutoka kwa wazazi, hivyo ni muhimu kujua historia na chanzo cha tatizo huku akiwaasa wazazi kutowapa watoto dawa za mafua na vikohozi bila ushauri wa daktari.



Dalili za tatizo

Dalili za nyama za pua zimeelezwa kuwa ni pamoja na mtoto kutoa makamasi mazito, kukoroma na mtoto kuacha mdomo wazi anapolala, kuongelea puani, kupata mafua ya mara kwa mara, kukohoa na kupata maumivu kwenye mfumo wa masikio.

Takwimu mahsusi za utafiti wa Hospitali ya Taifa Muhimbili uliochapishwa Agosti 2023 katika South Sudan Medical Journal ulibainisha kuwa watoto 420 waliopimwa katika hospitali hiyo walibainika kuwa na tatizo hilo. Kati ya wavulana walikuwa 218 sawa na asilimia 51.9 na wasichana 202 sawa na asilimia 48.1

Hali ikoje kweye nchi zingine

Ongezeko la watoto wenye matatizo ya ubongo na mfumo wa upumuaji kwa nchi zinazoendelea, kunahusishwa na wao kuwa karibu na harufu kali za manukato, hasa kwa wale wanaozaliwa mijini.

Wataalamu wa afya wanaeleza kuwa imethibitika kwamba watoto wachanga wanaponusa manukato, hasa yenye kemikali nyingi zaidi ya moja kwenye maukato, wanaweza kupata usonji (autism spectrum disorder).

Inaendelea Uk. 8

■ Habari Kuu

Manukato hatari...

Inatoka Uk. 7

Hivyo wanatoa tahadhari kwa wazazi, walezi na watu wengine wanaopenda kutumia manukato mengi kabla ya kuwabeba, kuwabusu au kulala karibu na watoto wachanga.

Kwa mujibu wa Chama cha Mapafu cha Marekani (American Lung Association), baadhi ya manukato huchanganywa na kemikali zinazoweza kuyeyuka na kusambaa hewani, zinazofahamika kitaalamu kama Volatile Organic Compounds (VOCs).

Kemikali hizo zinaweza kuchangia uchafuzi wa hewa ndani ya nyumba na kusababisha muwasho kwenye macho, pua na koo, kukohoa, kubanwa kifua au kupumua kwa shida.

Chama hicho kinaeleza kuwa watoto, wajawazito na watu wenye pumu au mzio ni miongoni mwa makundi yanayoweza kuathirika zaidi.

Hatari kwa mfumo wa upumuaji

Kwa watoto wachanga, harufu kali ya manukato inaweza kuchochea kubanwa kwa njia za hewa, hivyo kusababisha kukohoa, kupumua kwa mlilo wa mluzi na wakati mwingine kushindwa kupumua vizuri.

Chuo cha Marekani cha Madaktari Bingwa wa Mzio, Pumu na Kinga ya Mwili (ACAAI) kinazitaja harufu kali za manukato miongoni mwa vichochezi vya mashambulizi ya mfumo wa upumuaji kwa watoto.

Wakala wa Marekani wa Kulinda Mazingira (EPA) pia unaeleza kuwa baadhi ya kemikali zinazotumika kwenye bidhaa za kusafishia nyumba, vipodozi na manukato zinaweza kuchochea dalili za magonjwa ya mfumo wa upumuaji na hata kuathiri ukuaji wa ubongo.

Katika ushauri wake kwa wazazi, EPA inaelekeza kwamba watoto wasiwekwe karibu na bidhaa za manukato na zenye harufu kali na kwamba watoto walazwe ama kupumzishwa kwenye maeneo yenye mzunguko mkubwa wa hewa.

Hata hivyo, si kila mtoto anayenusu manukato atapata ugonjwa, na inaelezwa kuwa madhara hutegemea hali ya afya ya mtoto, aina ya bidhaa, kiwango cha kemikali na muda wa kukaribiana nazo.

Manukato yana uhusiano na usonji?

Miongoni mwa kemikali zinazochunguzwa kwenye manukato na vipodozi ni phthalates, ambazo zimethibitika kuwa na athari kwa watoto wadogo.

Inaendelea Uk. 9



**Mafundi wakien-
delea na ujenzi
wa mabanda ya
wafanyabiashara
pembezi mwa
barabara zilizopo
karibu na Sten-
di ya Daladala
Mbezi. Ujenzi huo
unafanywa na
Halmashauri ya
Manispaa ya
Ubungu,
Dar es Salaam.
(Na Mpigapicha
Wetu).**

Habari Kuu ■

Samia ateta na balozi wa Marekani



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na balozi mpya wa Marekani nchini, William Trachman, aliyefika Ikulu Jijini Dar es Salaam kuwasilisha hati za utambulisho mwishoni mwa wiki iliyopita. (Picha na Ikulu).

Manukato hatari...

Inatoka Uk. 8

Utafiti uliochapishwa mwaka 2021 katika jarida la Environment International, ukihusisha mama na watoto 501 nchini Marekani, ulichunguza uhusiano kati ya kemikali hizo wakati wa ujauzito na tabia za watoto walipofikisha umri wa miaka minne hadi mitano.

Watafiti walibaini uhusiano wa kitakwimu kati ya baadhi ya michanganyiko ya phthalates wakati wa ujauzito na ongezeko dogo la alama zinazopima sifa za kitabia zinazohusiana na usonji.

Utafiti mwingine wa mwaka 2018, uliochapishwa katika jarida la Environmental Health, uliwahusisha mama na watoto 201 kupitia mrandi wa Marbles nchini Marekani.

Watafiti hao walichunguza viwango vya phthalates katika mkojo wa wajawazito na kufuatilia ukuaji wa watoto wao.

Matokeo haya yalithibitisha kuwepo kwa kemikali hizo ambazo zilikuwa na athari kwa wajawazito na utambuzi wa usonji kwa watoto walipofikisha umri wa miaka mitatu.

Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha Marekani (CDC) kinaeleza kuwa usonji ni hali inayohusiana na tofauti za ukuaji na utendaji wa ubongo, na inaweza kuhusisha sababu mbalimbali za kijeni, kibaiolojia na kimazingira.

Madaktari washauri tahadhari

Chuo cha Marekani cha Madaktari wa Watoto (AAP) kinashauri familia kuchagua bidhaa zisizo na phthalates, baadhi ya kemikali nyingine zinazotia wasiwasi, au manukato ya kutengenezwa.

Katika mwongozo wake kuhusu bidhaa za matumizi binafsi, AAP kinashauri wazazi kuchagua bidhaa zenye maandishi fragrance-free, yaani zisizoongezwa kemikali za kutengeneza harufu, au zile zisizo na harufu kali.

Pia kinashauri kupunguza matumizi ya vipodozi kwa watoto wadogo, badala ya kuwapa-ka bidhaa nyingi zisizo za lazima.

Ushauri huo una maana kwamba wazazi wanapaswa kuwa waangalifu hata wanapotumia manukato wao wenyewe, hasa kabla ya kumbeba au kumnyonyesha mtoto mchanga.

Aidha, si lazima bidhaa yenye harufu ya maua au matunda iwe salama zaidi kuliko nyingine, kwa sababu kemikali zinazotengeneza harufu zinaweza kutoka kwenye mimea au kutengenezwa viwandani.

Wataalamu wa afya wanashauri pia kuepuka kunyunyizia manukato moja kwa moja kwenye ngozi, nguo, mito au matandiko ya mtoto, na kuhakikisha chumba anacholala kina hewa safi.

Ikiwa mtoto anaanza kukohoa, kubanwa kifua au kupumua kwa shida baada ya kukaribia harufu kali, mzazi anapaswa kumwondoa kwenye mazingira hayo na kutafuta ushauri wa kitabibu.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

Labda Baba wa Taifa angesema haya...



Mwalimu Julius Nyerere

OKTOBA 14, 2026 ilikuwa ni miaka 27 tangu Baba Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aondoke duniani.

Kwangu binafsi nina cha ziada. Ni siku ya kuzaliwa ya baba yangu mzazi, Mzee Benjamini Bagonza (1939-2025). Nyerere na Baba yangu wapumzike kwa amani.

Kitaifa kuna hisia zinazungumzwa chinichini. Baba wa Taifa alizoea kuziita “za kipumbavu.” Zinahusu ubaguzi. Kama angekuwa sasa, labda angesema haya yafuatayo.

Kwamba ipo chuki dhidi ya Ukatoliki ambayo inazidi kukua, lakini pia yapo mahaba kuhusu Ukatoliki. Yote mawili yanahitaji tahadhari.

Hatuwezi kumpenda mtu kwa sababu tu ni Mkatoliki bila kuwabagua wasio Wakatoliki. Mahaba huleta upofu na kustawisha ubaguzi.

Hatuwezi kumchukia mtu kwa kigezo cha Ukatoliki bila kuwapendelea wasio Wakatoliki

hata kama hawana sifa za uongozi.

Hatuwezi kujiona tunabaguliwa kwa Utanganyika au Ukristo wetu, bila kuwa na chuki ya ndani dhidi ya Uanzibari na Uislamu. Kinachokufanya ujione unabaguliwa kinaweza kukufanya uwabague wengine.

Hatuwezi kuwapendelea Wanzibari bila kwanza kutafuta sababu ya kuwabagua wasio Wanzibari. Mara nyingi kitu chepesi cha kutumia kuwabagua wasio Wanzibari ni dini.

Kigezo kinachounganisha makundi hayo hayo hapo juu ni dini. Tusisahau, dini kuu mbili hapa nchini, asili yake ni Ibrahimu. Ukimbagua Mkristo au Mkatoliki, Mwislamu au Mzanzibari, unakuwa umembagua Ibrahimu, baba wa imani yako. Bila Ibrahimu, dini yako unayotumia kubagua watu ni ushetani na maigizo matupu.

Awamu iliyopita, lilitokea wimbi la “Wachaga hao wasubiri.” Tukalichekea likaumiza watu. Mimi na baadhi ya wajinga wenzangu tukalike-mea. Tukatukanwa.

Sasa limekuja wimbi la hatutaki “Wakatoliki;” hawa wanajidai, wana viburi na wanadhani nchi hii ni yao peke yao. Tumekaa kimya kana kwamba hatuyasikii au kana kwamba hayapo.

Wanaoshinikiza hayo wanatamani nchi iwe yao peke yao. Dhambi ya ubaguzi wa dini, ubaguzi wa kiitikadi na ubaguzi wa eneo la Muungano havituachi salama.

Nawasihi tukemee hata dalili zake. Kama unafikiri ninazusha, jitambulisha wewe ni Mkatoliki au Mwislamu au Mtanganyika au Mzanzibari katika utumishi wako utajua ninachomaanisha. Neno “Mtanzania” limepelekwa jumba la Makumbusho ya Taifa.

Mungu analipenda sana taifa letu. Tusiombe aingilie kati kutuonyesha anavyolipenda. Tujifunze kuridhiana wenyewe kabla hajaingilia maugomvi yetu ya “kipumbavu.”

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Buriani Prof Mmari: Mtaaluma aliyeondoka tunapokumbuka miaka 27 ya Nyerere

OKTOBA 11, 2026, tuliondokewa na mtu mahiri, Profesa Geoffrey Mmari, mwanataaluma aliyelitimikia taifa katika sekta ya elimu na sekta nyingine mbalimbali kwa miongo mingi.

Kwangu ni wakati wa kutafakari maisha ya msomi na kiongozi ambaye nilipata fursa ya kufanya naye kazi na kujifunza kutoka kwake.

Kifo chake kimetokea siku chache kabla ya kumbukizi ya miaka 27 tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipofariki Oktoba 14, 1999.

Matukio haya mawili yanatualika kutafakari kuhusu aina ya watu tunaowahitaji katika kulijenga na kuliendeleza Taifa.

Nilimfahamu Profesa katika mazingira tofauti ya kazi. Alipokuwa anaanzisha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, nilikuwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na hapo tulishirikiana katika maandalizi ya uanzishwaji wa chuo hicho.

Nilipata nafasi ya kumfahamu katika mazingira ya kujenga taasisi kutoka katika hali ngumu kabisa. Hakuwa na hali ya kusubiri makuu pale anapotaka kutekeleza jambo, ilibidi akodishe basi dogo kutupeleka Nairobi Kenya kujifunza kuhusu Chuo Huria, fedha za tiketi za ndege zilipokosekana.

Wakufunzi 15 tulikwenda kujifunza na tulipokurudi tuliendelea katika kuanzisha Chuo hicho Huria.

Baadaye nilipokuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Profesa Mmari alikubali kuwa mwenyekiti wa Bodi ya Kituo kwa masharti ya kufahamu iwapo nafasi hiyo ina ukomo.

Alihudumu 2014 hadi 2019. Mambo muhimu niliyojifunza kutoka kwa profesa Mmari, ni kuthamini kazi na kufanya kazi kwa bidii, bila kupoteza muda.

Ninapomkumbuka Profesa Mmari katika kipindi hiki cha kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere ninatafakari misingi iliyowekwa na viongozi wanaoamini kuwa utumishi ni dhamana.

Profesa Mmari alikuwa mwalimu, msomi na kiongozi wa taasisi za elimu ya juu. Aliiongoza Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,

Chuo Kikuu Huria na Chuo Kikuu kishiriki cha KKKT Turdaco.

Pia aliongoza bodi za mashirika yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali kama Baraza la Habari na Kituo cha sheria na Haki za Binadamu.

Alishiriki kujenga na kuimarisha taasisi ambazo zinaendelea kuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya nchi yetu.

Wasifu wa Profesa Geoffrey Mmari hauishii katika orodha ya nyadhifa alizoshikilia. Kiongozi anapimwa si kwa nafasi alizoshika pekee bali ni kwa kuona athari za uongozi wake kwa watu na taasisi alizosimamia. Taarifa zilizotolewa baada ya kifo chake zinaelezea uadilifu wake, nidhamu ya kazi, unyenyekevu na namna alivyokuwa tayari kuwasikiliza wanafunzi na watenda kazi chini yake.

Tunaweza kuona ulinganifu wa maana na Mwalimu Nyerere aliyetambulika kwa msisitizo wake juu ya uadilifu, uwajibikaji, unyenyekevu na utumishi kwa wananchi. Kwake uongozi haukuwa nafasi ya kujinufaisha, bali dhamana ya kulitumikia taifa.

Kwa kuwaangalia watu hawa wawili tunaweza kujifunza kutokana na misingi inayowiana. Kwamba, nafasi ya uongozi inapaswa kuambatana na wajibu; heshima haiwezi kutenganishwa na tabia; maendeleo ya taifa yanahitaji watu wanaoweka maslahi ya taasisi na jamii mbele.

Kifo cha Profesa Mmari kitutafakarishe kuhusu elimu nchini. Tutaendelezaje taasisi zetu za elimu ya juu ziwe mahali pa kuzalisha maarifa, kulea viongozi wenye maadili na kutafuta majibu ya Changamoto zinazowakabili wananchi? Tuhakikisheje viongozi wanaoondoka madarakani wanaacha taasisi zenye misingi imara badala ya kutegemea uwepo wao binafsi?

Buriani Profesa Geoffrey Mmari, misingi uliyotuachia itaendelea kuishi.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240..

■ Habari

Mgongano wa maslahi upangishaji wa Hifadhi ya Barabara ya Morogoro



Moja ya vituo vya mafuta ambavyo ujenzi wake unaendelea kwa kasi ndani ya hifadhi ya Barabara ya Morogoro, jijini Dar es Salaam. (Na Mpiga Picha Wetu)

Na Waandishi WETU

KUMEIBUKA mvutano kuhusu upangishaji na matumizi ya Hifadhi ya Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam, huku Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) na Manispaa ya Ubungo wakitofautiana kuhusu mamlaka na nafasi ya kila upande katika usimamizi wa maeneo hayo.

Uchunguzi wa gazeti la Pambazuko umebaini kuwa maeneo ya hifadhi ya barabara kuanzia Kimara hadi Kiluvya yanazidi kutumiwa kwa shughuli mbalimbali za kibiashara, zikiwemo ujenzi wa vituo vya mafuta, maegesho ya malori, gereji, yadi za magari na baa.

Hali hiyo imebua maswali kuhusu utaratibu wa kutoa vibali, ushiriki wa mamlaka za serikali za mitaa na usalama wa uwekezaji unaofanyika katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi ya barabara.

Mjadala huo umeibuka wiki moja baada ya Pambazuko, katika toleo lake la Jumatatu - Oktoba 12, 2026, kuripoti kuhusu upangishaji wa maeneo hayo na malalamiko ya baadhi ya wananchi waliobomolewa nyumba za makazi na

biashara wakidai kutohusishwa katika mipango ya matumizi mapya ya maeneo hayo.

Kwa sasa, sehemu kubwa ya maeneo hayo inaendelezwa kwa shughuli za kibiashara, huku baadhi ya wawekezaji wakiendelea kujenga miundombinu ya kudumu ya biashara.

Manispaa yalalamikia kutoshirikishwa

Chanzo kutoka Manispaa ya Ubungo kiameiambia Pambazuko kuwa kutofautiana huko hakuhusu maeneo ya Kimara na Kiluvya pekee, bali pia maeneo mengine, yakiwemo yale yanayotumika kwa biashara ya kuuza magari.

Chanzo hicho kimetolea mfano wa eneo la Manzese, kikidai kuwa baadhi ya maeneo ambayo manispaa ilitarajia kuyasimamia yamepangishwa na Tanroads.

Kwa mujibu wa mtoa habari huyo, ingawa hifadhi za barabara ziko chini ya mamlaka ya Tanroads kisheria, bado kuna haja ya kuwepo kwa ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili ili kuratibu matumizi ya maeneo hayo na shughuli za biashara kwa sababu manispaa nayo inahusika kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa salama.

Chanzo hicho pia kimesema Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo aliandikia Tanroads Mkoa wa Dar es Salaam barua ya kuomba maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali, ikiwemo upangishaji wa wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga, lakini hadi wakati wa maelezo hayo, majibu yalikuwa hayajapatikana.

“Kimsingi tunapaswa kuwa na maeneo ya ushirikiano. Hatupaswi kugombana, lakini wenzetu wamepangisha hadi maeneo kwa manyesho na uuzaji wa magari yaliyopo kwenye hifadhi za barabara, kwa mfano maeneo ya Manzese na kwingineko,” kilisema chanzo hicho.

Inaendelea Uk. 13

Mgongano wa maslahi

Inatoka Uk. 12

Kiliongeza kuwa Tanroads inaonekana kutaka kusimamia maeneo hayo yote bila kuiachia manispaa nafasi ya kuyatumia katika shughuli zinazoweza kuongeza mapato ya halmashauri na kurahisisha usimamizi wa mazingira.

Ofisa mwingine ambaye hakutaka jina lake litajwe amesema kuna kutokubaliana kuhusu namna maeneo hayo yanavyopaswa kugawiwa na kusimamiwa, akidai kuwa baadhi ya maombi ya ushirikiano hayajapatiwa ufumbuzi.

Aidha, chanzo kingine kimesema baadhi ya maegesho ya malori yamepangishwa na Manispaa ya Ubungo, huku mengine yakisimamiwa na Tanroads. Kwa mujibu wa chanzo hicho, baadhi ya mikataba ya upangishaji inayohusishwa na Tanroads inafikia hadi Shilingi milioni 16 kwa mwaka.

Machinga nao wanatafuta nafasi

Kwa mujibu wa chanzo hicho, Manispaa ya Ubungo imekuwa ikitafuta maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, ikiwemo kuwatengea wafanyabiashara wadogo maeneo rasmi ya kufanyia biashara kuanzia Kiluvya hadi Daraja la Ubungo.

Chanzo hicho kimesema baadhi ya maeneo ya Kimara, Temboni na kituo cha daladala cha Mbezi, yanaendelea kuandaliwa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, ambao wanatarajiwa kupipa ushuru wa kati ya Shilingi 2,000 na 3,000 kwa siku. Gharama hizi zitategemea ukubwa wa eneo linalokodiwa.

Kwa upande mwingine, wawekezaji wanaotaka kujenga vituo vya mafuta au kuanzisha biashara nyingine katika hifadhi za barabara huwasilisha maombi Tanroads, ambayo hukagua eneo na kuweka masharti ya matumizi.

Chanzo hicho kimesema muda wa vibali unaweza kutofautiana kulingana na masharti yaliyowekwa, huku baadhi ya shughuli zikitarajiwa kuwa za muda na miundombinu yake iweze kuondolewa pale eneo linapohitajika kwa matumizi ya barabara.



Manispaa yakana mgogoro

Akijibu kuhusu madai ya kutokuelewana, Ofisa Habari wa Manispaa ya Ubungo, Jolina Nzali, amekana kuwepo kwa mvutano wa kugombea upangishaji wa maeneo hayo.

Amesema sheria inaelekeza wazi kuwa hifadhi za barabara ziko chini ya Tanroads.

Kuhusu madai kwamba manispaa imeandikia Tanroads kuomba maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo au kushirikiana katika usimamizi wa maeneo hayo, Nzali hakuthibitisha moja kwa moja suala la barua hiyo.

Amesema kuomba eneo kutoka kwa mamalaka nyingine hakumaanishi kwamba ombi hilo lazima likubaliwe.

“Sheria iko wazi. Maeneo hayo unayozungumzia yapo chini ya Tanroads, ingawa kwenye biashara sisi ndio wasimamizi,” amesema.

Ametolea mfano wa kituo cha daladala cha Mbezi, akisema uongozi wa wilaya uliwahi kuelekeza eneo la machininga lipangwe kwa kujenga vibanda vinavyofanana ili kudhibiti uchafu na kuondoa hali ya kila mfanyabiashara kujenga anavyotaka.

Tanroads wajitokeza kuzungumza

Kaimu Msimamizi wa Kitengo cha Matengenezo cha Tanroads Mkoa wa Dar es Salaam, Deogratus Lyatuu, amekiri kuwa baadhi ya maeneo ya hifadhi ya Barabara ya Morogoro yanaruhusiwa kutumiwa kwa shughuli mbalimbali za kibiashara, akisema hatua hiyo inatekelezwa kwa kufuata sheria na taratibu husika.

■ Habari

Mgongano wa maslahi

Inatoka Uk. 13

Lyatuu amesema matumizi hayo yanahitaji vibali na kwamba maombi ya wanaotaka kutumia maeneo hayo hupitiwa kabla ya kuidhinishwa.

“Kwa wanaohitaji kutumia hifadhi hiyo, utaratibu uko wazi. Wanawasilisha maombi yanayoeleza nia yao na eneo wanalotaka kulitumia. Maombi yanapitiwa na wanaokidhi masharti hupewa kibali cha muda, kwa masharti kwamba eneo likihitajika wakati wowote wataliachia na kulirejesha,” amesema.

Ameeleza kuwa vibali hivyo hutolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja na vinapaswa kuhishwa kila mwaka. Amesema utaratibu huo unatumika pia kwa baadhi ya biashara zinazohusisha vituo vya mafuta.

Kwa mujibu wa Lyatuu, utoaji wa vibali unazingatia Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zinazohusu matumizi ya hifadhi za barabara.

Amesema maombi hupitia mfumo rasmi ambao mwombaji hujisajili, na akitimiza masharti hupewa namba ya malipo ya serikali kabla ya kulipia na kukabidhiwa kibali.

Lyatuu ameongeza kuwa kibali cha matumizi ya eneo kutoka Tanroads si kibali pekee kinachohitajika. Kulingana na aina ya mradi, mwekezaji anaweza pia kuhitaji vibali kutoka Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), halmashauri husika na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), miongoni mwa taasisi nyingine.

Sheria inasemaje?

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, kinaeleza kuwa kimsingi hifadhi ya barabara imetengwa kwa ajili ya maendeleo na upanuzi wa barabara, pamoja na shughuli nyingine zinazohusiana na barabara.

Hata hivyo, sheria inaruhusu matumizi mengine kwa masharti maalumu - na hapa ndipo suala la upangishaji au utoaji wa vibali linapohitaji kuchunguzwa kwa makini.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, hifadhi ya barabara si eneo la matumizi holela ingawa mamlaka ya barabara inaweza kuruhusu matumizi ya muda katika eneo hilo.

Hata hivyo, sheria hiyo haina kifungu chochote kinachotoa ruhusa au mamlaka kwa taasisi yotote kukodisha eneo la hifadhi ya barabara.

Kifungu cha 29(2) kinaruhusu mamlaka ya barabara kutoa kibali cha maandishi kwa mtu au taasisi kutumia hifadhi ya barabara kwa muda kwa ajili ya huduma kama taa za umma, mawasiliano, matangazo, umeme, mifereji na mabomba ya maji taka au huduma nyingine zilizotajwa katika kifungu hicho.

Sharti muhimu ni kwamba matumizi hayo yasizuie matumizi ya baadaye ya eneo hilo kwa mahitaji ya barabara.

Usalama

Kuhusu usalama, Lyatuu amesema uwekezaji katika hifadhi za barabara hupaswa kuzingatia vigezo vinavyolenga kulinda watumiaji wa barabara. Kwa mfano, amesema vituo vya mafuta vinapaswa kuwa na njia za kuingia na kutoa kupitia barabara za huduma (service roads) badala ya kuingilia moja kwa moja barabara kuu.

Amesema matumizi rasmi ya maeneo hayo yanaweza pia kusaidia kuzuia uvamizi na kuongeza mapato ya Serikali kutokana na maeneo ambayo hayatumiki kwa shughuli za barabara kwa wakati huo.

Ameongeza kuwa utaratibu huo hautumiki katika Barabara ya Morogoro pekee, bali pia katika barabara nyingine za Dar es Salaam, ambako maombi ya matumizi ya maeneo ya hifadhi huwasilishwa kwa shughuli mbalimbali, zikiwemo maegesho ya magari na malori.

Uwekezaji wa muda au wa kudumu?

Pamoja na maelezo ya Tanroads kwamba vibali vinavyotolewa ni vya muda, uchunguzi wa Pambazuko umebaini kuwa baadhi ya maeneo yanayoendelezwa kwa biashara yanaonekana kuwa na miundombinu inayoweza kudumu kwa muda mrefu.

Inaendelea Uk. 15

Mgongano wa maslahi

Inatoka Uk. 14

Baadhi ya wawekezaji wanaojenga vituo vya mafuta wameonekana pia kujenga miundombinu mikubwa inayozunguka maeneo hayo, ikiwemo fremu za maduka ya kupangisha.

Hali hiyo imebua maswali kuhusu namna masharti ya vibali vya muda yanavyotekelezwa, gharama za uwekezaji na hatua zitakazochukuliwa endapo maeneo hayo yatahitajika kwa upanuzi au uboreshaji wa barabara.

Mwananchi mmoja aliyezungumza na gazeti hili amedai kuwa wakati wa utawala wa Rais wa zamani John Magufuli, msimamo ulikuwa kulin-da hifadhi za barabara zisijengwe kwa namna inayoweza kuzuia matumizi yake ya baadaye.

Ametoa mfano wa jengo la Tanroads lililopunguzwa sehemu yake, akisema hatua hiyo ililenga kuonesha umuhimu wa kuhifadhi maeneo ya barabara.

Mwananchi huyo ameonya kuwa uwekezaji mkubwa katika maeneo yanayotolewa kwa vibali vya muda unaweza kuwa na hatari ya kifedha ikiwa masharti yatabadilika au maeneo yatahitajika kwa matumizi mengine.

Amedai pia kuwa baadhi ya kampuni kubwa za mafuta huepuka uwekezaji wa aina hiyo, ingawa madai hayo hayajathibitishwa kwa maelezo kutoka kwa kampuni husika.

Ewura nayo yatoa kauli

Akizungumzia vituo vya mafuta vinavyojengwa katika maeneo hayo, Ofisa Habari Mkuu wa Ewura, Wilfred Mwakalosi, amesema Tanroads huingia makubaliano na waombaji kuhusu matumizi ya ardhi iliyopo ndani ya hifadhi ya barabara.

Amesema Ewura hufuata utaratibu wa kishe-ria kabla ya kutoa vibali vya ujenzi na uendeshaji wa vituo vya mafuta. Miongoni mwa hatua hizo ni kutangaza maombi ya vibali kupitia magazeti ili kuujulisha umma na kutoa nafasi kwa wenye pingamizi kuwasilisha maoni yao.

Mwakalosi amesema mwombaji anatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa kuruhusiwa kutumia eneo husika, cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira kutoka NEMC na cheti cha usalama kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Vilevile, mwombaji anapaswa kuwa na kibali cha ujenzi kutoka halmashauri husika pamoja na michoro iliyoandaliwa na mchoraji aliyeidhinishwa.

Amesema baada ya nyaraka hizo kuwasilishwa, Ewura hukagua kama masharti ya kisheria na kanuni yamezingatiwa kabla ya kutoa kibali kinachohusika.

“Ukiona ujenzi unaendelea mahali, ujue taratibu hizo zimezingatiwa na kwamba mwenye eneo, ambaye ni Tanroads, amekamilisha makubaliano yake na wahusika. Ewura inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria bila kuingilia mamlaka za taasisi nyingine,” amesema.



Lori likiwa limeegeshwa vibaya bila alama ya tahadhari katikati ya Barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam baada ya kuishiwa mafuta na kusababisha wengine wa barabara. (Na Mpiga Picha Wetu).

■ Uchambuzi

Makonda analaumiwa kwa lipi?



Na Mwandishi WETU

KUMEZUKA mjadala mkubwa wiki iliyopita baada ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Paul Christian Makonda, kuanza ziara ya siku kadhaa mkoani Mwanza kukagua miradi ya maendeleo.

Awali, kabla ya ufafanuzi kutolewa, ziara hiyo ilisababisha mkanganyiko kwa baadhi ya watu waliohoji kwa nini waziri anakagua miradi inayohusu wizara nyingine.

Baadaye ilibainika kuwa Makonda alikuwa akitekeleza jukumu lake akiwa mlezi wa Mkoa wa Mwanza, nafasi ambayo imekabidhiwa kwa baadhi ya mawaziri kwa lengo la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya maendeleo katika mikoa husika.

Chini ya utaratibu huo, tumewashuhudia mawaziri wengine wakifanya ziara zinazofanana.

Waziri wa Maji, Juma Aweso, amewahi kufanya ziara mkoani Manyara, huku Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa, akifanya ziara za kukagua shughuli za maendeleo mkoani Kili-manjaro.

Hata hivyo, ziara hizo hazikuibua mjadala mkubwa kama ule uliofuatia ziara ya Makonda.

Hali hiyo inazua swali; kwa nini ziara yake imeibua mjadala mkubwa kuliko za mawaziri wengine wanaotekeleza majukumu yanayofanana? Huenda hali hiyo inachangiwa na haiba au mtindo wa Makonda wa kutekeleza majukumu yake ya uongozi. Hata hivyo, badala ya kujikita katika mjadala wa haiba au tabia ya mtu, ni muhimu kuangalia mantiki ya serikali ya kuwakabidhi mawaziri jukumu la kulea na kusimamia maendeleo ya mikoa.

Kwa mtazamo huo, mjadala unaoendelea kuhusu ziara ya Makonda unatoa fursa ya kutathmini utaratibu huo, mamlaka zinazohusika na namna unavyoathiri uwajibikaji ndani ya Serikali.

Mgawanyo wa mamlaka, uwajibikaji

Utaratibu wa kuwateua mawaziri kuwa walezi wa mikoa unaweza kuibua maswali kuhusu mipaka ya mamlaka na mgawanyo wa majukumu ndani ya Serikali. Baadhi ya wachambuzi wanahoji iwapo mamlaka aliyonayo waziri kwa mujibu wa kiapo chake na majukumu ya wizara anayoisimamia yanaweza kutumika kushughulikia masuala yaliyo nje ya dhama yake ya moja kwa moja.

Waziri anapoapishwa, kiapo chake kinahusishwa na wadhifa wake na majukumu ya kusimamia sekta au eneo la kisera alilokabidhiwa.

Mamlaka yake ya kiutendaji hutokana na Katiba, sheria na mgawanyo wa majukumu ndani ya serikali.

Vivyo hivyo, wakuu wa mikoa wana majukumu yao ya kusimamia utawala na shughuli za Serikali katika maeneo waliyokabidhiwa, kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazohusika.

Uchambuzi ■

Mgongano wa maslahi

Inatoka Uk. 16

Kwa upande mwingine, Waziri Mkuu ana jukumu pana la kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali kwa mujibu wa Katiba na mgawanyo wa majukumu ya serikali.

Hapo ndipo swali la msingi linapojitokeza: ikiwa Waziri Mkuu ana wajibu wa kuratibu shughuli za serikali katika ngazi ya kitaifa, na wakuu wa mikoa wana jukumu la kusimamia shughuli za Serikali katika maeneo yao, nafasi ya mawaziri wanaoteuliwa kuwa walezi wa mikoa ni ipi?

Je, utaratibu huo unaimarisha uratibu na uwajibikaji, au unaongeza uwezekano wa majukumu kuingiliana na mamlaka kutokuwa wazi?

Maswali haya ni muhimu kwa sababu mfumo bora wa utawala unahitaji kila kiongozi kufahamu wajibu wake, mamlaka aliyopewa na namna atakavyowajibishwa kwa maamuzi yake.

Je, ziara nyingi zinaongeza tija?

Wakosoaji wa utaratibu huu wanaona kuwa kuongezeka kwa viongozi wanaokagua miradi ileile kunaweza kusababisha kurudiwa kwa ma-

jukumu na kupoteza muda na rasilimali ambazo zingetumika kutatua changamoto za wana-nchi.

Kwa lugha nyingine, utaratibu huo unaweza kufananishwa na miluzi mingi kwa mbwa wa mawindo: kila mmoja anatoa maelekezo, na matokeo yake unawexxa kumchanganya mbwa akashindwa kukamata mawindo sawasawa.

Katika mifumo ya utawala, kuna dhana inayojulikana kama chain of command, yaani mnyororo wa mamlaka na maelekezo unaofanua nani anawajibika kwa nani na kwa jambo gani. Mfumo huo ni nyenzo ya kuweka wazi uwajibikaji na kuzuia mkanganyiko na mwingiliano wa mamlaka.

Ikiwa kila kiongozi atajihusisha na kila jambo bila mipaka iliyo wazi ya majukumu, kuna hatari ya kupungua kwa ufanisi, kuchelewa kwa maamuzi na kutokuwa wazi kwa mhusika anayepaswa kuwajibika pale mradi unapokwama.

Kila waziri ana sekta au maeneo ya kisera anayopaswa kuyasimamia.

Bunge lina wajibu wake wa kutunga sheria, kuisimamia Serikali na kuiwajibisha. Kadhalika, viongozi wa mikoa na wilaya, makatibu tawala na mamlaka za serikali za mitaa wana majukumu yao katika usimamizi wa shughuli za maendeleo.

Kwa hiyo, ni muhimu kufahamu kama ziara za mawaziri walezi wa mikoa zina mfumo wa kuratibu matokeo na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo, au zinaishia kuwa matukio ya kukagua miradi bila mfumo unaopima manufaa yake.

Miradi mikubwa na matokeo

Jambo la msingi ni kwamba wananchi wanahitaji kuona matokeo na si uwepo wa viongozi wengi wanaosimamia maendeleo.

Wanahitaji miradi ikamilike kwa wakati, huduma za umma ziboreke na fedha za Serikali zitumike kwa tija.

Ziara za viongozi zinaweza kuwa na manufaa ikiwa zinalenga kubaini vikwazo, kuharakisha maamuzi, kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha miradi inakamilika kwa viwango vinavyotakiwa.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso



Stamico iliyotaka kuvunjwa sasa yavuna bilioni 147.8/-



Na Mwandishi WETU

SHIRIKA la Madini la Taifa (Stamico) limeongeza mapato yake ya ndani kutoka Shilingi bilioni 1.3 mwaka 2018/19 hadi bilioni 147.8 mwaka 2025/26.

Mafanikio haya yanaashiria mabadiliko makubwa katika uendeshaji wa shirika hilo linalomilikiwa kwa asilimia 100 na serikali.

Mafanikio haya yanapatikana kutokana na mageuzi makubwa yaliyofanywa ndani ya shirika hilo ambalo kwa nyakati tofauti - mara mbili serikali iliwahi kuliweka kwenye orodha ya mashirika ambayo yanapaswa kuuzwa.

Kwa mara ya kwanza, serikali ililiweka shirika hilo kwenye orodha ya mashirika yaliyopangwa kuuzwa mwaka 1997, wakati wa wimbi la ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

Aidha, mwaka 2019 serikali pia ilipendekeza shirika hilo livunjwe baada ya kufanya vibaya kwa muda mrefu.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Stamico, Dkt. Venance Mwasse, aliwaambia waha-

riri kuwa baada ya hapo yalifanyika mageuzi makubwa katika uendeshaji wa shirika kiasi kuwa hivi sasa limekuwa ni moja ya mashirika yanayojitegemea na kulipa gawio kwa serikali.

“Mafanikio hayo ni sehemu ya mageuzi yaliyolenga kuongeza ufanisi wa biashara, kupanua uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa madini na kupunguza utegemezi wa fedha za Serikali kwa ajili ya kuendesha shughuli za kawaida,” alisema Dkt. Mwasse.

Dkt. Mwasse, alieleza mafanikio hayo alipokutana na wahariri jijini Dar es Salaam Oktoba 16, 2026, katika mkutano ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina (OTR).

Alisema shirika limepanua shughuli zake za kibiashara, limeimarisha miradi inayomilikiwa moja kwa moja na kuongeza ushirikiano na wawekezaji katika miradi ya dhahabu, nikeli, grafiti na shaba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na Dkt. Mwasse, Stamico imeweza kugharamia matumizi yake ya kawaida kwa mapato ya ndani kwa miaka minne mfululizo, huku mishahara ya watumishi ikilipwa kutokana na mapato hayo kwa miaka mitatu sasa.

“Pamoja na hayo, shirika limeweza kutoa gawio kwa serikali na kupata hati safi za ukaguzi wa hesabu,” amesema Dkt. Mwasse.

Mapinduzi ya mapato na uzalishaji

Miongoni mwa mafanikio makubwa ya Stamico ni mabadiliko katika mwenendo wa mapato yake.

Takwimu zilizowasilishwa zinaonyesha kuwa mapato ya ndani yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 1.3 mwaka 2018/19 hadi bilioni 38.7/- mwaka 2021/22, bilioni 60.6/- mwaka 2022/23 na bilioni 72.2/- mwaka 2023/24.

Mwaka 2024/25, mapato yalikuwa Shilingi bilioni 68.8 kabla ya kupanda hadi bilioni 147.8/- mwaka 2025/26.

Biashara ■

Stamico iliyotaka

Inatoka Uk. 18

“Ukuaji huo umechangiwa na upanuzi wa shughuli za uchimbaji na biashara ya makaa ya mawe, huduma za uchorongaji, uzalishaji wa bidhaa za makaa ya mawe na kokoto, pamoja na miradi ya ubia katika madini mbalimbali,” alisema Dkt. Mwasse.

Katika biashara ya makaa ya mawe, anasema kuwa Stamico imefanikiwa kuugeuza mgodi wake wa Mchuchuma na Liganga kutoka kituo cha gharama na kuwa chanzo cha mapato.

Kwa mujibu wa mkurugenzi mtendaji huyo, mgodi huo uliendelea kuwa kituo cha gharama kati ya mwaka 2014 na 2020, kabla ya kuanza kuzalisha mapato kuanzia mwaka 2021.

Uzalishaji ulifikia tani 302,090 katika mwaka wa fedha 2025/26.

Uwekezaji miradi ya kimkakati

Dkt. Mwasse pia aliwaambia wahariri kuwa Stamico imepanua wigo wake wa uwekezaji kupitia miradi inayomilikiwa moja kwa moja na ile inayotekelezwa kwa ubia na wawekezaji binafsi.

Katika sekta ya dhahabu, alisema shirika linashiriki katika Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef kupitia ubia na TRX Gold Tanzania Limited.

Mgodi huo ulianza uzalishaji wa majaribio Julai 2020, ukiwa na mtambo wa awali wenye uwezo wa kuchakata tani tano za madini kwa saa. Kufikia Juni 2024, uwezo wa mtambo wa uchenjuaji ulikuwa umeongezeka hadi tani 90 kwa saa.

Katika sekta ya nikeli, Stamico inashirikiana na Coast Nickel Industry Limited kuendelea mradi wa Ntaka wilayani nachingwea mkoani Lindi.

Uzalishaji wa awali ulianza Desemba 2025, huku ujenzi wa kiwanda cha kuyeyusha nikeli eneo la Mlandizi, mkoani Pwani, ukifikia hatua za mwisho kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa.

Miradi mingine ya kimkakati ni pamoja na migodi ya dhahabu wa Kigosi, grafaiti huko

Mirerani na shaba huko Changube.

Shirika pia limesaini mikataba minne ya ubia inayohusu madini ya dhahabu, nikeli, grafaiti na shaba, pamoja na kupata leseni mpya 20 za madini ya kimkakati.

Kuimarisha wachimbaji wadogo

Mbali na uwekezaji wake wa moja kwa moja, Stamico imeendelea kutekeleza jukumu la kusaidia maendeleo ya wachimbaji wadogo, ambao wanakabiliwa na changamoto za mitaji, teknolojia, taarifa za kijiolojia na upatikanaji wa masoko.

Dkt. Mwasse anasema shirika limeanzisha huduma za uchorongaji na kununua vifaa vya utafiti wa jiosayansi ili kusaidia kubaini mashapo ya madini katika maeneo yenye leseni za uchimbaji mdogo.

Pia linashirikiana na Taasisi ya Jiolojia Tanzania (GST) katika tafiti za kijiolojia.

Kupitia vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Chunya, wachimbaji wadogo wanapata fursa ya kujifunza teknolojia bora na mbinu zenye tija zaidi za uchimbaji.

Katika suala la mitaji, Stamico imeingia makubaliano na benki za CRDB, NMB, Azania na KCB kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo.

Shirika pia linaunganisha wachimbaji na wanunuzi wa madini pamoja na wasambazaji wa vifaa vya uchimbaji.

Taarifa ya Stamico inaonyesha kuwa mchango wa wachimbaji wadogo katika mapato yatokanayo na sekta ya madini ulifikia asilimia 40 mwaka 2021/22. Hata hivyo, takwimu hiyo inatokana na utafiti wa kipindi hicho.



■ Habari

667,040 kufanya mtihani wa kidato cha nne leo



Katibu Mkuu Necta, Prof. Said Mohamed

Na Mwandishi WETU

JUMLA ya watahiniwa 667,040 wanatarajiwa kuanza mtihani wa kidato cha nne leo, Oktoba 19, 2026 hadi Novemba 6, 2026.

Watahiniwa hao watafanya mitihani katika vituo 7,067 nchini ikijumuisha shule za sekondari 6,265 na vituo 802 vya watahiniwa wakujitegemea.

Akizungumza na waandishi wa habari jana - Oktoba 18, 2026, Katibu Mtendaji wa Necta, Profesa Said Mohamed amesema kati ya watahiniwa waliosajiliwa, 644,085 ni wa shule, huku 22,955 wakiwa watahiniwa wa kujitegemea.

Amesema miongoni mwa watahiniwa wa shule, 910 wana mahitaji maalumu, wakiwemo wenye uoni hafifu 455, wasioona 13, wenye uziwi 98, wenye ulemavu wa akili 21 na wenye ulemavu wa viungo 323.

Kuhusu maandalizi, Profesa Mohamed amesema tayari baraza hilo limekamilisha maandalizi muhimu, yakiwemo mafunzo kwa wasimamizi na usambazaji wa vifaa vya mitihani katika halmashauri zote nchini.

Profesa Mohamed amesema mwaka huu idadi ya watahiniwa wa shule imeongezeka kwa 74,202, sawa na asilimia 13.02, ikilinganishwa na mwaka 2025, ambapo watahiniwa 569,883 walisajiliwa.

“Mtihani wa kidato cha nne ni muhimu kwa kuwa unapima umahiri wa watahiniwa katika yale yote waliyojifunza kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

“Pia matokeo ya mtihani huu hutumika katika uchaguzi wa watahiniwa wanaojiunga na kidato cha tano pamoja na fani mbalimbali za utaalamu,” amesema Profesa Mohamed.

Aidha, Profesa Mohamed amewaonya watahiniwa dhidi ya kujihusisha na vitendo vya udanganyifu, akisema matokeo ya watakaobainika kukiuka kanuni za mitihani yatafutwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Amewataka wamiliki na wakuu wa shule kutokuingilia majukumu ya wasimamizi katika kipindi chote cha mitihani.

Akizungumzia kuhusu endapo mvua za El-nino zinazotarajiwa kunyesha zitakwamisha mitihani hiyo, Profesa Mohamed amesema:

“Kamati zimeelekezwa kufanya kila njia ili wanafunzi wafanye mitihani na endapo itashindikana kabisa kwa mujibu wa kanuni watakaokwama watashiriki katika mitihani inayofuata.”

Kwa mwaka huu mitihani hiyo ya kidato cha nne inafanyika mapema tofauti na miaka yote, kutokana na tahadhari ya mvua za El-nino zinazotarajiwa kunyesha.

Uchambuzi ■

Mgongano wa maslahi

Inatoka Uk. 17

Lakini ikiwa viongozi wengi wanakagua mradi mmoja bila uratibu na bila kufuatilia utekelezaji wa maelekezo, manufaa ya ziara hizo yanaweza kuwa madogo.

Waziri Mkuu anabaki na jukumu gani?

Swali jingine linalostahili kujibiwa ni kuhusu nafasi ya waziri mkuu katika mfumo huu.

Ikiwa mawaziri walezi wa mikoa wanafanya ziara za kukagua miradi, waziri mkuu naye anafanya ziara za kukagua utekelezaji wa shughuli za serikali, na mawaziri wenye dhamana ya kisekta wanaendelea na ukaguzi wao, ni mfumo gani unaotumika kuhakikisha majukumu hayo yanaongezeana nguvu badala ya kurudiwa?

Zaidi ya hapo, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala, wakurugenzi wa halmashauri na viongozi wengine wa Serikali za mitaa nao wana wajibu wa kusimamia miradi na huduma za umma.

Pamoja na hayo pia zipo ziara za Mwenge wa Uhuru, Kamati za Bunge na viongozi wa kisiasa zinaweza kuongeza wigo wa ufuatiliaji.

Hata hivyo, ufanisi wake unategemea uwepo wa mipaka ya majukumu, uratibu wa taarifa na mfumo unaohakikisha kuwa mapungufu yanayobainika yanapatiwa ufumbuzi.

Bila mfumo huo, kuna hatari ya viongozi wengi kutumia muda kukagua miradi ileile huku changamoto za msingi zikiendelea.

Tunahitaji tija, si wingi wa ziara

Mjadala ulioibuliwa na ziara ya Makonda haupaswi kuishia katika kumlaumu au kumtetea mtu mmoja.

Unapaswa kuwa fursa ya kutathmini utaratibu mzima wa utawala na namna serikali inavyogawa majukumu ya kusimamia maendeleo.

Swali si kama waziri anaweza kutembelea mkoa au kukagua mradi unaotekelezwa na wizara nyingine pekee.

Swali la msingi ni kama ana mamlaka ya kufanya hivyo, kwa utaratibu gani, na hatua



Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa

anazochukua zinaongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya serikali. Taifa linahitaji viongozi wanaowajibika, mifumo inayoeleweka na watendaji wanaopima mafanikio kwa matokeo yanayoonekana kwa wananchi.

Hatimaye, serikali inapaswa kuweka wazi majukumu ya mawaziri walezi wa mikoa na uhusiano wao na waziri mkuu, mawaziri wa kisekta, wakuu wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa.


Hapo ndipo itakapowezekana kutathmini kama utaratibu huo unaongeza ufanisi au una-sababisha mwingiliano wa majukumu.



Rais Samia akiongoza kikao cha baraza la mawaziri

■ Makala ya Kilimo

Mustakabali wa kilimo Afrika si kuongeza mavuno pekee



Na Mwandishi MAALUM

MUSTAKABALI wa kilimo barani Afrika haategemei kuongeza mavuno pekee, bali pia kutumia mazao ya kilimo kujenga mnyororo wa thamani ya kiuchumi, ajira na ustawi wa wananchi kupitia uwekezaji, usindikaji na upatikanaji wa masoko.

Huo ni miongoni mwa mwelekeo unao-sisitizwa na Mtandao wa Afrika wa Taasisi za Utafiti wa Sera za Kilimo (ANAPRI), unaojumuisha taasisi 17 za utafiti wa sera za kilimo kutoka nchi 16 za Afrika. Katika mtandao huo Tanzania inawakilishwa na Ndaki ya Uchumi na Biashara (CoEBS) ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

ANAPRI inalenga kujenga uwezo wa taasisi wanachama na watafiti wake, huku ikiwezesha serikali kupata ushahidi wa kisayansi wa kuongoza maamuzi ya kisera na uwekezaji katika sekta ya kilimo.

Uzoefu kutoka Ghana na Malawi unaonyesha kuwa, pamoja na umuhimu wa kuongeza tija mashambani, mafanikio ya kilimo yanategemea pia mifumo madhubuti inayounganisha uzalishaji na uhifadhi, usindikaji, usafirishaji na masoko.

Hoja hizo zilijadiliwa katika kikao cha mfululizo wa semina za programu ya kuweka vipaumbele vya sera kwa kutumia uchambuzi wa mnyororo wa thamani (PPVC), kilichofanyika

kwa ushirikiano na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Sera ya Chakula (IFPRI) na Ofisi ya Sera ya Chakula na Kilimo (BFAP).

Programu hiyo inatekelezwa na taasisi wanachama wa ANAPRI kwa kushirikiana na IFPRI na BFAP katika nchi mbalimbali, zikiwemo Zambia, Ghana, Kenya, Tanzania na Malawi.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo, mbinu ya PPVC huchunguza mnyororo mzima wa thamani wa zao, kuanzia uzalishaji shambani hadi kumfikia mlaji, ili kubaini maeneo ambayo sera na uwekezaji vinaweza kuleta matokeo makubwa zaidi.

Nchini Zambia, kwa mfano, uchambuzi huo ulitumika kuongoza Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Mifugo. Katika majadiliano ya hivi karibuni, watafiti walichunguza changamoto na fursa katika sekta za nyanya na mpunga nchini Ghana, pamoja na zao la ndizi nchini Malawi.

Nyanya: Kupunguza upotevu na kuongeza thamani

Sekta ya nyanya nchini Ghana inaonesha changamoto zinazoweza kujitokeza pale mahitaji ya soko yanapoongezeka bila kuwepo kwa mifumo imara ya uzalishaji, uhifadhi na usindikaji.

Miongoni mwa changamoto zinazokabili sekta hiyo ni upotevu wa mazao baada ya kuvunwa, uhifadhi usioridhisha na uwezo mdogo wa viwanda vya kusindika nyanya.

Hali hiyo husababisha sehemu ya thamani inayozalishwa mashambani kupotea kabla bidhaa hazijawafikia walaji.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, watafiti wanapendekeza mabadiliko katika mifumo ya umwagiliaji na kuwekza zaidi kwenye mifumo inayotegemea zaidi nishati ya jua. Hii itasaidia kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kumnufaisha mkulima.

Inaendelea Uk. 23

Makala ya Kilimo ■

Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Taasisi za Utafiti wa Sera za Kilimo Afrika (ANAPRI), Profesa Andrew Temu, akikata utepe kuzindua ofisi za mtandao huo katika Jiji la Lusaka, nchini Zambia hivi karibuni (Na Mpiga Picha Wetu).



Mustakabali wa kilimo

Inatoka Uk. 22

Pia unahitajika utafiti wa mbegu zinazostahimili magonjwa na kwa kiasi kikubwa kuanzishwa kwa vituo vidogo vya usindikaji ili kuhakikisha kuwa mkulima anapata soko la uhakika la mazao yake.

Mapendekezo mengine ni kujenga maghala maalumu kwa ajili ya kupokea na kupanga mazao, kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao katika mazingira ya baridi na kuboresha mbinu za kushughulikia mazao baada ya kuvunwa.

Hatua hizo zinalenga kupunguza upotevu, kuongeza thamani ya nyanya na kuhakikisha kuwa bidhaa zinafika sokoni katika hali inayokidhi mahitaji ya walaji.

Mpunga: Uzalishaji uendane na mahitaji ya soko

Kwa upande wa mpunga, uzoefu wa Ghana unaonesha changamoto ya pengo kati ya ongezeko la mahitaji ya mchele na kasi ya uzalishaji wa ndani.

Matumizi ya mchele kwa kila mtu nchini humo yameongezeka mara mbili katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, huku uzalishaji wa ndani ukishindwa kukua kwa kasi inayolingana na ongezeko la mahitaji. Hali hiyo imeongeza utegemezi wa Ghana kwa mchele unaoagizwa kutoka nje.

Lakini uzoefu huo unaonesha kuwa ili kupunguza utegemezi wa bidhaa za chakula kutoka nje, haitoshi kuongeza uzalishaji wa mpunga pekee. Ni muhimu pia kuimarisha uwezo wa ndani wa kusindika mpunga kuwa mchele wenye ubora unaokidhi mahitaji ya soko.

Hivyo, uwekezaji katika usindikaji na mifumo ya usambazaji ni sehemu muhimu ya juhudi za kuongeza ushindani wa mchele unaozalishwa nchini humo.

Ndizi: Umuhimu wa miche bora

Nchini Malawi, changamoto zinazokabili sekta ya ndizi zinaonesha umuhimu wa kuanza mageuzi ya kilimo kwa kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mbegu na miche bora.

Inaendelea Uk. 30

■ Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

Ofisa Uhusiano sio spika ya matangazo

HUKU kwetu tuna kawaida moja. Tunajenga nyumba kwanza, halafu tunamwita mhandisi aje aeleze kwa nini kuta zinapasuka.

Ufa ukishatoka dirishani mpaka sakafuni ndipo mtu anakumbuka kwamba kuna mtu alisomea mambo haya.

Taasisi zetu nyingi zinawachukulia wataalamu wa mawasiliano hivyo hivyo.

Uamuzi unafanyika Jumatatu katika chumba cha mikutano, milango imefungwa. Jumatano mtu anafungua mlango na kupaza sauti korido nzima; “Yuko wapi mtu wa PR? Tunahitaji taarifa kabla ya saa kumi.” Taarifa inatoka. Wananchi wanaipokea vibaya. Ijumaa, walewale ambao hawakuomba ushauri wanauliza kwa nini mawasiliano yameshindwa.

Oktoba 8, 2026 pale Dodoma, Chama cha Mao-fisa Uhusiano na Mawasiliano Tanzania (PRST) kiliadhimisha miaka 10 kwenye Mkutano Mkuu na Tuzo za Umahiri katika Uhusiano na Umma na Mawasiliano.

Miaka kumi inastahili sherehe, lakini pia inastahili swali gumu; miaka kumi ijayo itatuletea nini?

Savera Salvatory Kazaura, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, aliyetoa hotuba ya Mgeni Rasmi, hakuzunguka.

Aliwataka viongozi wa taasisi za umma na binafsi kuwashirikisha wataalam Uhusiano na Umma tangu hatua za awali za kupanga na kufanya maamuzi, badala ya kuwatumia kutangaza maamuzi ambayo tayari yamefanyika.

Uhusiano na Umma, alisema, ni zaidi ya taarifa kwa vyombo vya habari na kuratibu matukio.

Kauli hii imetoka ndani ya serikali yenyewe. Natumaini wale waliopaswa kuisikia walikuwepo ukumbini.

Mantiki ni rahisi. Mtaalamu wa Mawasiliano aliyekuwepo kabla ya uamuzi atakwambia nani ataguswa kwanza, upinzani utatoka wapi, maneno gani yataeleweka vibaya, na mgogoro gani unakaribia kuutengeneza kwa mikono yako mwenyewe.

Aliyeitwa baada ya uamuzi anaweza tu kuchagua aina ya herufi za kuandikia habari mbaya.

Kazaura alionya kuhusu kasi ya taarifa potofu mitandaoni, na teknolojia zinazoweza kutengeneza au kubadilisha picha na sauti.

Hili sio tatizo la Tanzania peke yake. Ni la Afrika na dunia nzima. Sauti ya uongo iliyotengenezwa kwa Akili Unde haiulizi una cheo gani.

Imani haijengwi wakati wa mgogoro. Inajengwa siku za kawaida kabla yake, kupitia taarifa sahihi, majibu kwa wakati, uwazi, na juu ya yote, viongozi ambao matendo yao yanaendana na maneno yao.

Kazaura pia alisisitiza kwamba mawasiliano lazima yawe ya pande mbili. Taasisi zisitoe taarifa tu, bali zisikilize, zijibu maswali na zichukue hatua juu ya changamoto za wananchi.

Hapa ndipo wengi tunajidanganya. Tunatoa taarifa tunaita mawasiliano. Tunatrendi mchana mmoja tunaita ushirikishwaji.

Lakini je, watu waliuelewa uamuzi? Viongozi waliielewa kinachowasumbua watu? Kuna maoni hata moja yaliyobadilisha chochote? Kama hapana, hatukuwa tunawasiliana. Tulikuwa tunatangaza.

Dkt. Mary Hospicia Kafyome, Makamu Rais mstaafu wa PRST, alieleza kwamba chama kimeandaa na kuwasilisha rasimu ya sheria ya kuweka mfumo rasmi wa kusimamia taaluma, yenye viwango vinavyotambulika, maadili yanayosimamiwa na utambuzi wa kitaaluma.

Mchakato bado unaendelea, haujawa sheria. Aliongeza kwamba taaluma hii ina nafasi katika kufanikisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kwa kujenga uelewa wa wananchi juu ya mipango ya maendeleo.

Lakini sheria pekee haitafungua mlango wa bodi. Dkt. Kafyome mwenyewe alikiri kwamba bado tunahitaji kushirikishwa zaidi katika maamuzi ya kimkakati, kufanya utafiti zaidi na kupima matokeo ya kazi zetu.

Baada ya miaka kumi, changamoto yangu ni rahisi. Kwa viongozi: acheni kuwaita wataalamu wa mawasiliano pale tu kuta zinapopasuka. Kwa wataalamu: leteni takwimu, busara na maadili yatakayowafanya msiweze kuachwa nje.

Kiongozi anayewaita wataalamu wa mawasiliano kutangaza uamuzi tu hatafuti ushauri. Anatafuta spika.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@loth-makuza.co.tz

Na Emmanuel JACOB



Afya ya Kimwili ■

Kutegemea virutubisho pekee haitoshi kutibu 'arthritis'



KATIKA jamii zetu, watu wengi wanaotesea na maumivu makali pamoja na kukaza kwa viungo yaani "arthritis" wamekuwa wakikimbilia kutumia virutubisho au tiba lishe wakitafuta nafuu ya haraka.

Chupa zenye nembo za kuvutia zinazoahidi kurejesha ute ute kwenye viungo na kujenga upya collagen zilizoharibika zimejaa kwenye maduka ya dawa.

Hata hivyo, wataalamu wa afya wanaonya kuwa kutegemea bidhaa hizi kama tiba mbadala ya kudumu ni dhana potofu na hatari.

Ukweli ni kwamba virutubisho pekee haviwezi kutibu arthritis, wala haviwezi kurejesha upya viungo vilivyokwisha haribika kabisa.

Ili kufanya uamuzi sahihi kuhusu afya yako, ni muhimu kutofautisha kati ya matangazo ya biashara na ushahidi wa kisayansi.

Dhana kwamba virutubisho vinaweza kujenga upya collagen au kutibu kabisa ugonjwa huu haina mashiko ya kitiba. Ingawa bidhaa kama glucosamine au chondroitin husemwa kusaidia maumivu ya magoti na nyonga, tafiti kubwa zinaonyesha matokeo mchanganyiko ambapo watumiaji wengi hawapati nafuu yoyote zaidi ya athari ya kisaikolojia.

Pia kuna uelewa mdogo kuhusu usalama wa bidhaa hizi. Mara nyingine watu wengi huamini kuwa kwa kuwa bidhaa ni ya asili, basi ni salama kutumia kiasi chochote. Hata hivyo, virutubisho havidhibitiwi kwa umaakini mkubwa na vyombo vya udhibiti wa dawa.

Kutumia dozi kubwa kunaweza kusababisha madhara au kuingiliana vibaya na dawa za shinikizo la damu, kisukari, na zile za kuyeyusha damu.

Zaidi ya hayo, kuacha kufanya mazoezi na kumpumzisha kiungo kwa muda mrefu hufanya misuli kudhoofika na kuongeza ukakamavu.

Pamoja na changamoto hizo, baadhi ya virutubisho hutoa nafuu ya muda kupunguza maumivu vikitumiwa kwa usahihi.

Kwa mfano, mafuta ya samaki yenye Omega-3 husaidia kupunguza uvimbe na kukakamaa viungo hasa asubuhi kwa wenye rheumatoid arthritis.

Vilevile, viambata vya manjano kama curcumin na mti wa boswellia vimeonekana kufanya kazi sawa na dawa za kutuliza maumivu kama ibuprofen. Nayo SAM-e inasaidia kupunguza uvimbe huku ikiboresha hisia na msongo wa mawazo kwa wagonjwa.

Mwisho kabisa, kutegemea virutubisho pekee huweka afya yako hatarini kwa sababu haviwezi kuchukua nafasi ya matibabu ya hospitali.

Usumamizi mzuri wa arthritis unahitaji mbinu jumuishi ikiwemo kuzingatia dawa, kufanya mazoezi ya viungo ili kuimarisha misuli, kuongeza uweza wa kukunja na kunyoosha kiungo na kuendelea kuwa mchangamfu.

Kabla ya kuanza au kutumia kirutubisho chochote, ni vyema kupata ushauri wa daktari ili kujilinda dhidi ya madhara ya madawa.

Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob

Bustani ya Sheria



Na Wakili Karim Gabriel Mussa

Hatua kabla ya kukamilisha muamala wa kununua ardhi



BAADA ya kufanya uchunguzi wa ardhi na kusaini mkataba wa mauziano, mnunuzi na muuzaji huingia katika hatua nyingine muhimu inayojulikana kwa Kiingereza; pre-completion stage.

Hatua hii inahusisha kutimiza masharti ya kifedha na kisheria yanayotakiwa kabla ya kukamilisha uhamisho wa umiliki wa ardhi.

Miongoni mwa mambo yanayopaswa kushughulikiwa ni kodi na tozo zinazohusika na muamala.

Hizi zinaweza kujumuisha kodi ya mapato inayotokana na mauzo ya mali (Capital Gains

Tax), ushuru wa stempu (Stamp Duty) na mali-po mengine yanayotakiwa kulingana na aina ya ardhi na mazingira ya mauziano.

Ni muhimu kuelewa kwamba wajibu wa kulipa kodi fulani unaweza kumhusu muuzaji au mnunuzi kutegemea sheria inayotumika.

Vilevile, kiwango cha kodi hakipaswi kuchukuliwa kuwa sawa katika kila muamala; kinapaswa kuthibitishwa kwa kuzingatia sheria na tathmini inayokubalika na mamlaka husika.

Katika hatua hii, wahusika wanapaswa kuanadaa nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya tathmini, ulipaji wa kodi na uhamisho wa umiliki.

Nyaraka hizo zinaweza kujumuisha mkataba wa mauziano, ripoti ya tathmini, maombi au tarifa za kuhamisha haki ya ardhi na hati ya umiliki, kutegemea mahitaji ya mamlaka husika.

Aidha, ni muhimu kuthibitisha kama kodi ya ardhi inayodaiwa imelipwa na kupata uthibitisho wa malipo yanayotakiwa. Kwa upande wa kodi ya mapato inayotokana na mauzo, wahusika wanapaswa kufuata utaratibu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuwasilisha nyaraka zinazohitajika na kupata uthibitisho wa malipo pale kodi inapodaiwa.

Somo la Kisheria; Usidhani kwamba kusaini mkataba kunamaanisha ununuzi wa ardhi ume-kamilika.

Hakikisha kodi na tozo zinazotakiwa zime-lipwa, nyaraka zimekamilishwa na masharti ya uhamisho wa umiliki yametimizwa kabla ya kuhitimisha muamala.

Katika ununuzi wa ardhi, umakini katika hatua hii unaweza kukuepusha na uchelewesha-ji, gharama zisizotarajiwa na migogoro ya kisheria.

Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karim-binmussa@gmail.com

AI yaweza kugeuka janga kwa binadamu

TUKIO la programu ya akili unde (AI) kushambuliwa na wahalifu wa mtandao na kusababisha halijoto katika jokofu za supermarket kupanda hadi nyuzi joto 80, na hivyo kuyeyusha baadhi ya samani na kuharibu bidhaa, linaibua maswali mengi.

Moja ya maswali hayo na muhimu zaidi ni hili; binadamu ana udhibiti kiasi gani juu ya teknolojia anayoizalisha?

Katika tukio hilo, lililoripotiwa kupitia maelezo ya mwathirika, supermarket nchini Ufaransa ilikabiliwa na hasara kubwa baada ya mifumo yake ya kidijitali kuvamiwa.

Kilichoanza kama shambulio la mtandao kiligeuka kuwa tatizo la kimwili, likionyesha jinsi udhaifu wa programu unavyoweza kuathiri vifaa na shughuli za kila siku.

Hatari kubwa zaidi ni kwamba matukio kama haya yanaweza kuvuka mipaka ya biashara na kuathiri hospitali, mifumo ya umeme, usafirishaji na huduma nyingine muhimu kwa maisha ya binadamu.

Hapa ndipo mjadala kuhusu AI unapokuwa wa dharura. Kadiri mifumo hiyo inavyopata uwezo mkubwa wa kufanya uamuzi na kutekeleza majukumu bila usimamizi wa karibu wa binadamu, ndivyo madhara ya hitilafu, matumizi mbaya au mashambulizi yanavyoweza kuongezeka.

Wataalamu wanaonya kuwa mifumo ya AI yenye uwezo mkubwa inaweza kufanya mambo ambayo hata watengenezaji wake hawawezi kueleza au kuyadhibiti kikamilifu.

Tatizo si kwamba kila mfumo una nia ya kudhuru, bali ni kwamba wakati mwingine matokeo ya uamuzi wake, mifumo hii inaweza kuwa mgumu kuitabiri na kuidhibiti.

Hatari nyingine ni kasi ya maendeleo ya teknolojia hiyo. Mifumo ya kisasa inaweza kusaidia kuandika programu, kuchambua taarifa na kuboresha michakato ya kiteknolojia.

Ikiwa AI itapewa jukumu kubwa zaidi katika kutengeneza au kuboresha mifumo mingine ya AI, bila ukaguzi wa kutosha, makosa yanaweza kuenea kwa kasi ambayo binadamu atashindwa kuisimamia ipasavyo.

Tayari dunia imeshuhudia mashambulizi ya mtandao yakisababisha hospitali kuahirisha huduma, kampuni kupoteza mamilioni ya fedha na mifumo ya huduma muhimu kuvurugika.

Ingawa si matukio yote hayo yaliyosababishwa na AI, yanaonesha madhara yanayoweza kutokea pale teknolojia muhimu inapokuwa katika mikono isiyo sahihi.

Suluhisho si kuizuia AI kabisa. Teknolojia hii ina uwezo wa kuboresha tiba, elimu, kilimo na uzalishaji. Kinachohitajika ni kuhakikisha kuwa kasi ya maendeleo yake haiishii kuizidi kasi ya uwezo wetu wa kuidhibiti.


Serikali zinapaswa kuweka kanuni madhubuti, kampuni kuwa wazi zaidi kuhusu hatari za mifumo yao, na wataalamu huru kupewa nafasi ya kuipima kabla haijaingizwa katika huduma nyeti.

Mifumo inayodhibiti umeme, vifaa vya hospitali na miundombinu mingine muhimu inahitaji ulinzi wa ziada na uwezekano wa kuzimwa kwa usalama pale hitilafu inapotokea.

Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania, maandalizi hayo ni muhimu sasa, kabla matumizi ya AI hayajapanuka zaidi.



Maendeleo ya AI yasipimwe kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi zaidi pekee, bali pia kwa uhakika wa binadamu kwamba anaweza kuizuia inapokosea.

Kwa sababu teknolojia ambayo binadamu hawezi kuisimamia inaweza kugeuka kutoka kuwa chombo cha maendeleo na kuwa chanzo cha hatari kubwa kwa maisha na uchumi.



■ Uchambuzi

Tunamkumbuka Nyerere kwa picha, fikra na ndoto zake?



Na Prim-Innocent MUNGY

MIKA 27 imepita tangu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere atuache.

Wiki iliyopita, hususan Oktoba 14 ambapo taifa lilisherehekea siku ya Mwalimu Nyerere, tulishuhudia picha zake zikiwa zimesambaa kila sehemu tukimkumbuka, maneno yake ya-karudiwa na jina lake likatajwa kwa heshima.

Hali hii hutokea kila mwaka wakati wa mkumbukizi yake.

Hotuba za viongozi zinakuwa nyingi, huku wakijinasibu kuwa wanamuenzi Nyerere!

Lakini uzoefu unaonyesha kuwa tukimaliza tu kumkumbuka inaishia hapo. Baadhi tunaji-uliza; tunarudi kuishi namna gani?

Kwa baadhi yetu tuliokuwa tukimsikiliza Mwalimu Nyerere, tukimuuliza maswali magumu, kumbukumbu yake inabeba matumaini ya Tanzania ambayo mtoto wa kila Mtanzania ange-weza kusoma, mgonjwa anghudumiwa kwa utu, na kiongozi angesikia shida ya mwananchi kama wajibu wake.

Je, sasa tunaishi ndoto hizo, au tumezoea kuzisimulia?

Tunapomwona kijana mwenye uwezo akikata tamaa kwa kukosa nafasi, mzee akihangaika kupata huduma, au mtu akinyimwa haki kwa sababu hana wa kumsema, tunaweza kweli kusema tumemuenzi Mwalimu?

Kumkumbuka kwa uaminifu kunahitaji ujasiri wa kujitazama. Inawezekana hakuwa mkamilifu, na si kila alichotarajia kilitimia, lakini hilo halituondolei wajibu wa kujiuliza tulichofanya na matumaini aliyotuachia.

Tumejenga uwezo wa kujitegemea kiasi gani? Umoja wetu una nafasi kwa wenye mawazo tofauti? Nafasi tulizo nazo zinapunguza shida za watu au zinaongeza umbali kati yetu?

Maswali haya yanamhusu pia kila mmoja wetu; ofisini, nyumbani, katika biashara na katika namna tunavyoyaishi maisha yetu.

Huenda umuhimu mkubwa wa kumbukizi hii ungekuwa kuona picha yake ukutani, huku mtu anayehitaji haki akimfikiria Mwalimu chini yake.

Miaka 27 baadaye, heshima tunayompa Mwalimu ionekane katika maisha ya watu. Hapo ndipo kumbukumbu yake itakapokuwa hai.

Namuomba heri Mwalimu Nyerere na aendelee kupumzika kwa amani Baba wa Taifa!

Barua za Wasomaji ■



Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz

Tumuenzi Mwalimu Nyerere kwa vitendo

Mhariri,

OKTOBA 14, kila mwaka Tanzania huadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ambaye alifariki dunia siku hiyo mwaka 1999.

Ni miaka 27 sasa bila baba wa taifa, kiukweli naanza kuona siku hii watu wakianza kuipuuza na kutokuichukulia kwa uzito uleule kama ilivyokuwa awali. Siku ya Mwalimu Nyerere haipaswi kuwa tu siku ya mapumziko kitaifa watu kutokwenda makazini, bali siku hii tuitumie kama ya tafakuri ya kitaifa kwa kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo na kuziishi nasaha zake. Naomba turudishe utaratibu uleule wa kumuenzi Mwalimu kama zamani, nakumbuka ilikuwa ikifika Oktoba 1 tu tunaanza kuona hotuba za Mwalimu Nyerere katika kila luninga.

Binafsi namkumbuka Mwalimu Nyerere katika harakati za kudai uhuru, kupambana na ujinga, maradhi na umasikini, alikemea rushwa, udini na ukabila waziwazi na alisisitiza hilo.

Pia tuwafundishe watoto wetu umuhimu wa waasisi wa taifa hili na mchango wao.

Hassan Kindole, Gangilonga, Iringa.

Kongole Makamu wa Rais Ndejembu

Mhariri,

HIVI karibuni Makamu wa Rais, Deogratius Ndejembu alitoa wazo kuhusu vijana kuajiriwa na Shirika la Umeme nchini (Tanesco) huku akisema kama serikali ikibana matumizi wanaweza kuokoa pesa na ikatumika kuwaajiri vijana 10,000 nchi nzima.

Wiki iliyopita Tanesco wakatanga-za ajira kwa vijana 1,000 katika kada mbalimbali. Hakika huu ni mwanzo mzuri kwa makamu wetu wa rais.

Ombi langu kwa serikali iendelee kubana matumizi ili ajira 10,000, alizotamani makamu wa rais ziweze kufikiwa.

Kongole Ndejembu mwanzo mzuri, Tanesco wametekeleza agizo lako kwa vitendo.

Jema Joseph,

Kiteto, Manyara.

Matukio ya watu kuuana ni afya ya akili?

Mhariri,

HIVI karibuni kumekuwa na matukio mengi ya ukatili yanayowahusisha watoto wadogo wa shule ya msingi kujinyonga pamoja na wanandoa kuuana kikatili, hali hii inatisha na kadri siku zinavyozidi kwenda janga hili linazidi kuota mizizi na kuwa sugu.

Matukio matatu katika mikoa ya Morogoro, Mwanza na Katavi ya wanafunzi kujinyonga yamenifanya kuandika barua hii. Huko Morogoro, wanafunzi wa darasa la nne mwenye umri miaka 11 alijinyonga kisa baba yake alicheleweshewa pesa ya kununulia kalamu ya mtihani, mwingine wa miaka 10 alijinyonga pia, kisa bibi yake alimhoji kuhusu madaftari mkoani Mwanza.

Mwanafunzi mwingine miaka 11 naye alijinyonga kisa baba yake alichelewa kutoa pesa ya mchango wa shilingi 10,000 mkoani Katavi.

Swali ambalo najiuliza nini kinaendelea katika jamii yetu hadi watu wanakosa utu kiasi hichi, je ni tatizo la afya ya akili, msongo wa mawazo au ndio ugumu wa maisha unachangia matukio ya namna hii kuwa mengi. Serikali kupitia wizara ya afya pamoja na wizara ya elimu, waanzishe programu mahsusi kwa ajili ya kutoa elimu juu ya tatizo la afya ya akili katika jamii.

Pia waanzishe somo maalum la saikolojia ianzie ngazi ya shule ya msingi hadi chuo kikuu.

Emmaculate Johnson, Kisesa, Mwanza.

■ Makala ya Kilimo

Mustakabali wa kilimo

Inatoka Uk. 23

Uzalishaji wa ndizi nchini humo uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mlipuko wa ugonjwa unao sababishwa na virusi vya Banana bunchy top virus (BBTV), ambao ulisababisha uharibifu mkubwa wa mashamba ya migomba.

Uzoefu huo unaonesha umuhimu wa kuwekeza katika upatikanaji wa miche bora na salaama, pamoja na kuimarisha mifumo ya kudhibiti na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mimea.

Kwa ujumla, uchambuzi wa ANAPRI unasisitiza kuwa serikali na wadau wa kilimo wanapaswa kutekeleza hatua zinazopendekezwa kwa mtazamo jumuishi, badala ya kuzichukulia kama miradi inayojitegemea. Uzalishaji, usindikaji, uhifadhi na masoko vinapaswa kuimarishwa kwa pamoja ili kuongeza manufaa ya kiuchumi yanayotokana na kilimo.

Kupanua wigo wa utafiti wa sera

Uchambuzi wa minyororo ya thamani ni mojawapo tu ya maeneo ya utafiti yanayofanywa kazi na ANAPRI.

Mwaka huu mtandao huo umefanya tathmini ya haraka ya athari za mgogoro wa Mashariki ya Kati katika mifumo ya chakula ya nchi nane, zikiwemo Tanzania, Kenya na Ethiopia.

Aidha, unaendeleza kampeni ya Mkulima, Ujue Udongo Wako kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD). Pia unaandaa mpango wa bara zima wa kuimarisha minyororo ya thamani ya mahindi, mchele, ngano na mbegu za mafuta, pamoja na jukwaa la kutoa ushauri wa haraka wa kisera kwa serikali.

Katika kuimarisha uwezo wa watafiti wa Afrika, ANAPRI inapanga kuanzisha programu ya ufadhili na ukuzaji wa watafiti (Fellowship) kuanzia Novemba 2026.


Kupitia programu hiyo, watafiti kutoka taasisi wanachama watapata usimamizi na mafunzo katika uchambuzi wa uchumi mzima, uchambuzi wa masoko mahususi (Partial Equilibrium Analysis) na uchambuzi wa minyororo ya thamani.

Lengo ni kuhakikisha kuwa ujuzi huo unajengeka na kubaki ndani ya taasisi za Afrika.

Masuala hayo yanatarajiwa kujadiliwa katika Mkutano wa 13 wa Wadau wa ANAPRI utakao-fanyika Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia Oktoba 26 hadi 30, 2026. Mkutano huo utakuwa na kaulimbiu isemayo, "Kujenga Uchumi Shindani wa Kilimo na Chakula: Sera, Biashara na Njia za Uchumi wa Viwanda kwa Afrika."

Mwenyekiti wa Bodi ya ANAPRI, Profesa Andrew Temu, amesema lengo la mtandao huo ni kujenga taasisi inayotegemewa na serikali za Afrika kwa kutoa ushauri wa kitaalamu unao-tegemea ushahidi na suluhisho madhubuti kwa changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo na mifumo ya chakula.

Kwa msingi huo, uzoefu wa Ghana, Malawi na Zambia unaonesha kuwa mustakabali wa kilimo Afrika unahitaji zaidi ya kuongeza uzalishaji. Unahitaji sera zinazotegemea ushahidi, uwekezaji unaolenga maeneo yenye matokeo makubwa na mifumo inayohakikisha kuwa mazao yanayozalishwa yanahifadhiwa, yanaongezewa thamani na kufikishwa sokoni kwa ufanisi.



Wafanyabiashara ya ndizi wakisubiri wateja katika Soko la Mabibo, Dar es Salaam baada ya kushushwa kwa wingi na malori kama walivyokutwa na kamera ya Pambazuko juzi. Wengi wa bidhaa hiyo umesababisha kushuka kwa bei hadi Shilingi 25,000 kwa mkungu kutoka bei ya awali ya Shilingi 50,000.

Makala ya Kimataifa ■

Somalia na Somaliland: Mgogoro wenye dhana ya nchi dhaifu - I



Rais wa kwanza wa Somalia, Mohamed Siad Barre

Na Mwandishi MAALUM

KATIKA mfululizo wa makala za Gazeti la Pambazuko zinazochambua masuala mbalimbali ya kisiasa na kimataifa, leo tunaangazia mgogoro kati ya Somalia na Somaliland, historia yake na maslahi ya kimkakati yanayolizunguka eneo hilo.

Watu wengi huenda wasifahamu tofauti iliyopo kati ya Somalia na Somaliland. Tofauti hizo zinatokana na historia, mifumo ya utawala na hadhi yao katika jumuiya ya kimataifa, licha ya wakazi wa maeneo hayo kuwa na lugha na tamaduni zinazofanana kwa kiasi kikubwa.

Historia ya Somalia na Somaliland

Mji Mkuu wa Somaliland ni Hargeisa. Eneo hilo lilikuwa chini ya utawala wa Uingereza kabla ya kupata uhuru Juni 26, 1960.

Siku chache baadaye, Julai 1, 1960, liliungana na eneo lililokuwa chini ya utawala wa Italia na kuunda Jamhuri ya Somalia.

Hata hivyo, baada ya kuanguka kwa serikali kuu ya Somalia mwaka 1991, Somaliland ilitangaza kujitenga na kurejesha uhuru wake wa awali.

Tangu wakati huo, imekuwa ikijitawala kwa kiwango kikubwa, ikiwa na taasisi zake za kisiasa na kiutawala, huku ikiendelea kutafuta kutambuliwa kimataifa kama taifa huru.

Kwa upande mwingine, Somalia ina mji mkuu wake, Mogadishu na serikali ya shirikisho, bunge pamoja na taasisi za usalama.

Somalia inatambuliwa kimataifa kuwa taifa huru na ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU).

Serikali ya Shirikisho ya Somalia inaendelea kulisitiza kuwa Somaliland ni sehemu ya eneo lake, wakati viongozi wa Somaliland wakisisitiza haki yao ya kujitawala kama taifa huru.

Kwa nini eneo hili lina umuhimu?

Hata hivyo, suala la Somaliland haliishii katika mjadala wa mipaka na mamlaka ya kisiasa.

Eneo hilo pia linahusishwa na maslahi mapana ya kiuchumi, kibiashara na kijeshi kutokana na nafasi yake kijiografia kwani ipo karibu na Ghuba ya Aden, Bahari Nyekundu na mlango bahari wa Bab al-Mandab.

Hili ni eneo muhimu sana kwa usafirishaji baharini.

Swali muhimu katika uchambuzi wa kijiografia na kisiasa unapaswa kuwa; ni kwa kiwango gani udhibiti wa njia hizi za baharini unaweza kuathiri usalama wa biashara ya kimataifa na ushindani wa mataifa yenye maslahi katika ukanda huo?

Bab al-Mandab ni njia nyembamba ya baharini inayounganisha Ghuba ya Aden na Bahari Nyekundu.

Inaendelea Uk. 32

■ Makala ya Kimataifa

Somalia na Somaliland: Mgogoro wenye dhana..

Inatoka Uk. 31

Kupitia njia hiyo, meli zinaweza kuelekea Mfereji wa Suez na kuendelea hadi Bahari ya Mediterania, hivyo kuwa sehemu muhimu ya biashara inayounganisha Asia na Ulaya.

Kwa mujibu wa Tawala ya Taarifa za Nishati ya Marekani (EIA), takribani mapipa milioni 9.3 ya mafuta ghafi na bidhaa za mafuta yalipitia Bab al-Mandab kwa siku mwaka 2023.

Kiasi hicho kilipungua hadi wastani wa mapipa milioni 4.1 kwa siku mwaka 2024, huku kukiwa na changamoto za kiusalama zilizo-changia meli kubadili njia zake za usafirishaji.

Takwimu hizo zinaonesha umuhimu wa njia hiyo katika biashara ya nishati duniani, pamoja na namna migogoro ya usalama inavyoweza kubadili mwenendo wa usafirishaji wa bidhaa.

Jiografia na sifa za Bab al-Mandab

Bab al-Mandab iko kati ya Yemen upande wa Rasi ya Arabia na Djibouti pamoja na Eritrea upande wa Afrika.

Kijiografia, njia hiyo inaunganisha Bahari Nyekundu na Ghuba ya Aden, ambayo ni sehemu ya Bahari ya Arabia.


Kisiwa cha Perim, kinachojulikana pia kama Mayyun, kiko ndani ya mlango bahari huo na kuugawa katika njia mbili za kupitisha meli.

Nafasi yake inaongeza umuhimu wa kijiografia wa eneo hilo katika usafiri wa baharini.

Jina Bab al-Mandab ni neno la kiarabu lnye maana “Mlango wa Machozi” au “Mlango wa Maombolezo”. Jina hilo linahusishwa na simulizi za kihistoria kuhusu hatari za kuvuka eneo hilo.

Mbali na umuhimu wake wa kibiashara, ukanda huo umekuwa ukikabiliwa na changamoto za kiusalama, zikiwemo mashambulizi dhidi ya meli, uharamia na athari za migogoro ya kikanda.

Hata hivyo, ni muhimu kutofautisha uharania wa baharini na mashambulizi ya kisiasa au kijeshi dhidi ya meli, kwa kuwa matukio hayo yanaweza kuwa na sababu na wahusika tofauti.



*Rais wa Somalia
Hassan Sheikh
Mohamud*

Uwepo wa majeshi na ushindani wa mataifa

Umuhimu wa Bab al-Mandab umechangia mataifa mbalimbali kuweka vikosi na vituo vya kijeshi katika nchi zinazozunguka ukanda huo, hususan Djibouti.

Miongoni mwa mataifa yenye uwepo wa kijeshi nchini humo ni Marekani, China, Ufaransa, Japan na Italia.

Vituo hivyo vina majukumu mbalimbali, yakiwemo shughuli za kijeshi, ufuatiliaji wa usalama wa baharini, kupambana na uharamia na kusaidia operesheni za kikanda.

Uwepo wa vikosi hivyo pia unaonesha maslahi mapana ya mataifa hayo katika usalama wa Bahari Nyekundu, Pembe ya Afrika, Mashariki ya Kati na Bahari ya Hindi.

Hata hivyo, uwepo wa vituo hivyo haupaswi kutafsiriwa moja kwa moja kuwa mataifa yote yana lengo moja au yanashirikiana katika operesheni zinazofanana. Kila nchi ina maslahi, makubaliano na vipaumbele vyake vya kiusalama.

Inaendelea Uk. 33

Makala ya Kimataifa ■

Somalia na Somaliland: Mgogoro wenye dhana..

Inatoka Uk. 31

Kwa hiyo, ushindani wa kimkakati katika eneo hilo unapaswa kuchunguzwa kwa kuzingatia sera za nje za mataifa husika, mikataba ya kijeshi na hatua zinazochukuliwa katika kulin-da biashara na usafiri wa baharini.

Utambuzi wa Somaliland na maslahi ya kimataifa

Katika muktadha huo, suala la kutambuliwa kwa Somaliland limeongeza mjadala kuhusu uhusiano kati ya mamlaka ya kisiasa, usalama wa kikanda na maslahi ya kimataifa.

Israel iliitambua Somaliland kama taifa huru Desemba 26, 2025, hatua iliyopokelewa kwa mitazamo tofauti. Serikali ya Somalia imeikataa hatua hiyo, ikisisitiza kuwa Somaliland ni sehemu ya eneo lake.

Umoja wa Afrika nao umeendelea kuisisitiza umuhimu wa kuheshimu umoja, mamlaka na mipaka inayotambulika kimataifa ya Somalia.

Kwa mtazamo wa kimkakati, hatua hiyo inaweza kuchambuliwa kwa kuzingatia nafasi ya Somaliland karibu na Ghuba ya Aden na Bab al-Mandab, pamoja na uwezekano wa kuimarika kwa ushirikiano wa kidiplomasia, kiuchumi na kiusalama kati ya pande husika.

Migogoro ya kikanda na athari zake

Migogoro ya Yemen, ikiwemo mapigano yanayohusisha makundi yenye silaha na mashambulizi dhidi ya meli, imeongeza changamoto za usalama katika eneo la Bahari Nyekundu na Ghuba ya Aden.

Hali hiyo imeathiri maamuzi ya kampuni za usafirishaji kuhusu njia za kupitisha mizigo na gharama za bima.

Kwa upande wa Somalia, miongo kadhaa ya mapigano, udhaifu wa taasisi za serikali na changamoto za kiusalama vimeathiri uwezo wa nchi hiyo kusimamia kikamilifu masuala ya ndani na maslahi yake ya kimataifa.

Katika mazingira hayo, Somaliland imejenga mifumo yake ya utawala na kiusalama, jambo linalochangia mvuto wake katika mjadala ya kidiplomasia na kiuchumi.


Hata hivyo, utulivu wa eneo hilo, maslahi ya mataifa ya nje na suala la hadhi yake ya kimataifa ni masuala tofauti yanayohitaji kuchambuliwa kila moja kwa ushahidi wake.

Kwa hiyo, mgogoro kati ya Somalia na Somaliland hauwezi kueleweka kwa kuangalia historia ya kujitenga pekee.

Ni muhimu pia kuchunguza nafasi ya eneo hilo katika biashara ya kimataifa, usalama wa baharini na uhusiano wa mataifa yenye maslahi katika Pembe ya Afrika.

Sehemu ya pili ya makala hii itaendelea wiki ijayo.





Thamani ya wazazi hailingani na chochote



HABARI za leo wasomaji wangu wa safu hii ya uhusiano yenye lengo la kuihabarisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kimaisha.

Mada ya wiki hii inahusu umuhimu wa wato-kujali na kuthamini mchango wa wazazi wao.

Wazazi ni watu muhimu kuliko kitu chochote katika maisha ya binadamu.

Kwa lugha ya picha, mzazi anaweza kufananishwa na mizizi ya mti. Mti unaweza kuwa na maua mazuri, matunda matamu na majani mazuri, lakini bila mizizi hauwezi kudumu, hufa.

Wazazi ndio msingi wa uhai wa mtoto bila kujali umri wake. Hakuna chuo, hakuna kazi, hakuna ndoa ambayo ingekuwepo bila wazazi.

Mama anabeba mtoto wake kwa maumivu, baba alilinda uhai wako kabla hujafahamu maa-na ya dunia. Hilo pekee linatosha kuwafanya watoto kuwaenzi wazazi wao milele.

Wao pia ni shule ya kwanza. Kabla ya mwalimu, mama ndiye aliyemfundisha mtoto wake kuzungumza maneno mbalimbali kama vile mama, asante na baba alifundisha kusimama baada ya kuanguka, maadili, heshima, uvumilivu na vyote walivifundisha kabla ya kuanza shule.

Wazazi ni benki isiyo na riba kwani unaweza kukosa pesa na ukasahauliwa na watu wote wakiwemo ndugu lakini mzazi atafanya jitihada za kukupatia hata senti ya mwisho aliyobakiwa nayo bila kukuandikia deni.

Wao pia ni baraka; machozi ya mama yanap-

okudondokea kwa furaha, ni baraka, maneno ya baba mfano 'nimekuridhia mwanangu' yanafungua milango ambayo digrii haiwezi kuifungua.

Wao pia ndio historia yako kwani bila wao hakuna binadamu ambaye atakuwa kitu kwani wanafahamu kila kitu na bila wao huwezi kuwa kitu.

Ikitokea wazazi wako wanafariki dunia huwezi kuishi kwa amani na furaha duniani kwa kuwa unakuwa umepoteza kitu muhimu katika maisha yako ingawa kuna wakati unaweza kusahau taratibu machungu ya kuondokewa nao.

Lakini katika dunia ya sasa watoto wengi wamekuwa mwiba kwa wazazi wao kutokana na kuwaacha bila msaada wowote, jambo lina-lowafanya wazazi walio wengi kusunoneka.

Wengi wao huwatelekeza wazazi wao bila kuwasaidia kwa kuwapatia chochote na wengi wao huachwa wakiwa dhaifu kutokana na uzee, magonjwa yanayotokana na hali zao na mengineyo na kusahau fadhila walizopata kutoka kwao walipokuwa chini yao.

Wazazi ni baraka inayopita haraka. Tuwajali na kuwalipa mema wakiwa hai.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Mitindo & Urembo ■



'Waistcoat'; mtindo unaobamba kwa wanawake

WAISTCOAT ni mtindo wa koti lenye mikono mifupi ambayo, kwa siku za karibuni imekuwa ikivaliwa sana na wanawake wa kisa-sa.

Mtindo huu unaweza kuvaliwa kwa staili nyingi ikiwemo rasmi na "casual."

Kwa vazi rasmi; unaweza kuvaa koti hili juu ya shati lenye mikono mirefu huku chini ukipigilia na suruali au sketi ya suti na kiatu kirefu.

Kwa mtoko wa casual; unaweza kuvalia na top au yenyewe kwa kufunga vifungo vyake.



Tumia scrub hii kung'arisha ngozi

WATU wengi hawana utaratibu wa kutumia scrub zaidi ya kupaka tu mafuta.

Lakini ukweli ni kwamba scrub zina umuhimu katika kung'arisha ngozi yako na kuwa na afya.

Leo nakuletea scrub yenye mchanganyiko wa sukari, kahawa, manjano na asali.

Mambo ya kuzingatia;

* Changanya kijiko kimoja cha sukari, kahawa kijiko kimoja, manjano kijiko kimoja na asali.

* Changanya mchanganyiko wako vizuri halafu ipake usoni iache kwa dakika tano kisha safisha uso wako vizuri.

* Kwa matokeo mazuri, hakikisha unatumia kila siku kwa wiki mbili mfululizo.

■ Burudani



Majizzo asikitishwa wanaodharau muziki wa singeli

Na Mwandishi WETU

MKURUGENZI Mkuu wa EFM na TVE, Francis Ciza maarufu Majizzo, ameeleza kusikitishwa na namna baadhi ya watu wana-vyodharau muziki wa singeli.

Majizzo amesema muziki wa singeli unahitaji mata-masha makubwa, wadhami-ni na ushirikiano wa wadau ili kuendelea kukua kama ilivyo kwa Bongo Fleva. Kutokana na hilo, amewataka wadau wa singeli kuungana na kuutetea muziki huo badala ya kukata tamaa, akisisitiza kuwa bado kuna nafasi ya kuufanya uendelee kukua



Msigwa: Tumieni ushindi wa Jihan kama fursa

Na Mwandishi WETU

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amewataka Watan-zania kutumia fursa zitaka-zotokana na ushindi wa Jihan Dimack pamoja na Tanzania kuwa mwenyeji wa mashin-dano ya Miss World 2027. Msigwa ametoa wito huo juzi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, alipokwenda kumpokea Jihan, aliyerejea nchini baada ya kutwaa taji la Miss Grand International 2026.

Jihan amekuwa Mtan-zania na Mwafrika wa kwanza kushinda taji hilo. Akizungumzia maandalizi ya Miss World 2027, Msigwa alisema timu kutoka uongozi

wa mashindano hayo tayari ipo kwa ajili ya maandalizi, huku Tanzania ikiwa imelipa ada zinazohitajika.

Amesema vikao vinaendelea na serikali ita-anzisha utaratibu utakaow-awezesha wadau kushiriki. Msigwa amewahimiza wa-nanchi waanze kufikiria namna ya kunufaika na matukio hayo makubwa. Amesema Jihan atakuwa na taji lake kwa mwaka mzi-ma, hivyo wenye mawazo ya shughuli au miradi in-ayoweza kufanyika katika kipindi hicho wayawasil-ishe kwa uongozi wake au wizarani ili yafanyiwe kazi. Miss Grand International, ambayo Jihan ameshinda, ni mashindano tofauti na Miss World 2027, ambayo Tan-zania imepata haki ya kuwa mwenyeji wake.

Michezo Kimataifa ■

Kwa Yanga hii, ni mnara uliosimama, mtandao haushiki!

Na John MARWA

LICHA ya kuibuka na ushindi katika mchezo wa mkondo wa kwanza hatua ya Lawali Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF CL), Yanga, bado hawana furaha kwa namna timu yao inavyocheza hivi sasa, mashabiki ni minuno na lawama tu.

Yanga walishuka dimbani Oktoba 17 kumenyana na wenyeji wao klabu ya CFFA ya Magadascar, mchezo uliochukua nafasi katika Uwanja wa Azam Complex, Mbade Chamazi, ambapo CFFA waliuchagua kuwa uwanja wao wa nyumbani katika mchezo huo.

Haukuwa mchezo wa kuvutia kwa mashabiki kwa namna walivyoutazama hasa kipindi cha kwanza, licha ya kuwa dakika 90 zilihitimika kwa wenyeji CFFA kupokea kipondo cha mabao 0-4.

Mabao ya Yanga yaliwekwa kambani na Shekhe Toure, Kangwanda, Mudathir Yahya na Maxi Nzengeli na kuhitimisha ujenzi wa mnara wa 4G ambao bado mtandaoni wa furaha haushiki kwa Wananchi.

Kwa ushindi huo Yanga wametanguliza mguu mbele katika hatua ya makundi ya CAF CL msimu huu ambapo mchezo wa marudiano ni wikiendi hii pale pale Uwanja wa Azam Complex ambapo Yanga ni wenyeji katika mashindano hayo ya kimataifa.

Ikumbukwe kuwa ushindi huo ni mara baada ya kutoka kuteseka kwa kipondo kutokana kwa watani zao wa jadi, Simba, mchezo wa Ligi Kuu ya Tanzania uliochalazwa Oktoba 10 mwaka huu.

Kipigo hicho kwa Yanga ni kama kimewavuraga Wananchi, kila mmoja haoni jema la timu yake hata kama mnara unasoma.

Lawama za mashabiki zinaelekezwa kwa Kocha Mkuu Manqoba Mngqithi na benchi lake la



ufundi kwa ubora wa kikosi hicho kushuka kwa mujibu wa maono yao na jinsi wanavyoitathimini timu yao mara baada ya kufungwa na Simba.

Ushindi huo wa Yanga kwa timu ya Madagascar, ni sawa na kusimamisha mnara, lakini mtandao hausomi, isipokuwa tu walipata kinachohitaji katika mchezo ambayo ni matokeo ya ushindi, lakini mtandao wa furaha, mawimbi hayashiki.



Mnyama na pori lake la maajabu



Na John MARWA

WAKATI mbonga bado haijaisha ndani, furaha ya wana Simba kuwa katika kilele chake, wakiwa wana ng'ata minofu tu, Mnyama anaingia tena mawindoni katika pori lake la maajabu; Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF CL), kupambana na 15 de Agosto de Akonibe ya

Equatoria Guinea.

Katika mchezo huo, Simba atakuwa ugenini Oktoba 21, majira ya saa tisa alasiri katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam, ambapo wenyeji wao wamechagua uwanja huo kutumika kwa mtanange huo wa mkondo wa kwanza kuwania kutinga hatua ya makundi CAF CL.

Wenyeji wa mchezo huo, wakiwa wanatambua makucha ya Mnyama kuwa ni mashabiki wake, wametia ngumu mashabiki kuwa sehemu ya burudani hiyo, hivyo wenye Simba yao watalaazimika kutoka ndani ya mwitu na kutazama mtanange huo kupitia television.

Je, 15 de Agosto, kukataa mashabiki wataweza kumfinyia Mnyama kwenye chaka lake la maajabu? Ni swali ambalo majibu yake yatapatikana ndani ya dakika 90 za mchezo huo kabla ya kurejea kwa wana Lunyasi hao katika mchezo wa marudio ambapo Simba watakuwa wenyeji.

Ni wazi utakuwa mchezo mgumu kwa sababu, mpira wa miguu ni mchezo wa maajabu.

Simba wakiwa katika ubora wao, watabinya kitufe cha hatari ama watambembebeza mwana apite hadi ndani?

Macho ya wapenda soka na wahafidhina wa soka wanatamani kuona nini kitatokea, kutoka pande zote za Afrika, mashaka yao ni kwa 15 de Agosto kama watamtimua Mnyama kwenye window lake?

Hakika ni mchezo ambao hakuna jicho litatamani kufumba kwa namna ambavyo Simba wamekuwa na muendeleo wa matokeo bora, na kiwango cha kuvutia msimu huu katika mashindano yote wanayoshiriki.